# IKULU ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 025 ISSN 1821 - 8253 MEI - JUNI 2016




# Sherehe za siku ya wafanyakazi - Mei Mosi

- Serikali imejidhatiti kuendelea kuimarisha maslahi ya wafanyakazi
- Shirikisho la vyama huru la wafanyakazi lapongeza juhudi za Serikali
- Vyasisitiza kuwa haki na wajibu ni watoto pacha

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu**
Hassan K. Hassan

**Mhariri Msaidizi**
Ali S. Hafidh

**Waandishi**
Said J.Ameir
Rajab Y. Mkasaba
Haji M. Ussi
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Mahfoudha M. Ali
Amina M. Ameir

**Mpiga Picha**
Ramadhan O. Abdalla

**Msanifu**
Aziz I. Suwed


## UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.


Jarida hili limetolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.



P.O.BOX: 2422
Zanzibar - Tanzania
Phone: +255 223 0814/5
Fax: 024 223 3722
Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz


# Maoni ya Mhariri

## Kutoa taarifa kwa umma ni jukumu la kila kiongozi wa Serikali

Katika zama hizi za utawala wa kidemokrasia ambao unahimiza uwazi na uwajibikaji, suala la mawasiliano kati ya Serikali na wananchi limekuwa sio tu ni sehemu ya utawala, bali ni utamaduni katika uendeshaji wa Serikali duniani kote.

Kwa nchi zilizoendelea suala la mawasiliano tayari limeshakuwa utamaduni uliozoeleka tofauti na nchi zetu zinazochipukia katika mifumo ya siasa za ushindani. Hata hivyo, pamoja na kupewa kipaumbele, suala hili la mawasiliano bado halijafanikiwa sana katika nchi za zinazoendelea.

Katika kuhakikisha kuwa Zanzibar haibaki nyuma katika suala hilo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kujenga mifumo madhubiti ya kuwezesha mawasiliano bora na ya uhakika kati yake na wananchi pamoja na washirika wengine.

Mawasiliano kati ya Serikali yanafanyika kwa njia nyingi ikiwemo matumizi ya vyombo vya habari, mikutano ya hadhara ya viongozi na wananchi na washirika wa Serikali pamoja na matumizi ya njia za kisasa za teknolojia ya habari na mawasiliano kama vile tovuti na mitandao ya kijamii.

Lakini mfumo wa mawasiliano umejengwa katika misingi ya ushirikiano kati ya mtoa taarifa, mchukuaji taarifa na walengwa. Na kwa sababu ni mawasiliano, bila ya shaka kunakuwepo na mrejesho miongoni mwa wanaowasiliana.

Tokea baada ya Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari 1964, kumekuwepo na jitihada mbalimbali za kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa suala la Serikali kuwasiliana na wananchi. Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa tangu awamu ya kwanza ya uongozi hadi awamu hii ya saba ili kujenga mazingira bora zaidi ya kuwezesha mawasiliano hayo.

Mawasiliano na umma ni moja kati ya ajenda muhimu katika Serikali ya awamu ya saba inayoongozwa na Dk. Ali Mohamed Shein. Kwa hakika tangu kuingia madarakani mwaka 2010 amefanya jitihada kubwa kuhakikisha kuwa kunakuwepo na mawasiliano ya karibu kati ya Serikali anayoiongoza na wananchi wakati wote.

Tungependa kukumbusha katika ukurasa huu kuwa lengo kuu la Serikali kuwa na mawasiliano na wananchi ni kuhakikisha wananchi wanashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo kwa kupewa taarifa muhimu ambazo zitawasaidia kufahamu mipango ya Serikali, utekelezaji wake na nafasi yao katika kushiriki utekelezaji wa mipango hiyo.

Kwa kuwa pande hizo zinawasiliana ni rahisi kwa Serikali kuwafahamisha wananchi kile ambacho imekusudia kukifanya, lengo lake na manufaa yake kwa wananchi na nchi kwa jumla. Kwa upande mwengine, Serikali kwa kutumia njia nzuri za mawasiliano, itaweza kufahamu nini hasa mahitaji halisi ya wananchi na changamoto zao na hivyo kuchukua hatua zinazofaa kwa wakati muafaka.

Katika kuhakikisha suala hilo linafanyika kwa ufanisi mkubwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba imetoa muongozo unaowahimiza viongozi wote wa Serikali wakiwemo Mawaziri, Makatibu wakuu, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutoa taarifa kwa wananchi kila baada ya kipindi maalum kuhusu utekelezaji wa shughuli zao. Hii ni kwa sababu watumishi wote wa umma wanawajibika kwa wananchi.

Mheshimiwa Rais amekuwa mfano bora katika kutekeleza hili la kuwasiliana na wananchi mara kwa mara. Amekuwa akikutana na wananchi na kuzunguza nao ana kwa ana katika hadhira mbalibali, lakini pia anawasiliana nao kupitia mikutano yake na waandishi wa habari.

Wakati Mheshimiwa Rais anaonekana kuweko mstari wa mbele katika kulitekeleza hilo, bado viongozi na watendaji wengi wa Serikali wamekuwa wagumu kutekeleza mkakati wa Serikali wa mawasiliano.

Tatizo hili limekuwa ndio kilio kikubwa cha waandishi wa habari kila wanapokutana na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Katika mazungumzo yake na waandishi wa habari hivi karibuni hoja hiyo ilijitokeza kwa mara nyengine tena ambapo Mheshimiwa Rais alijibu kwa ufupi kwa kusema "suala hilo halihitaji tena mjadala, tulitoa mwongozo tangu mwaka 2011. Viongozi na watendaji husika hawapaswi kukataa kutoa habari kwa vyombo vya habari".

Safu hii inapenda kusisitiza kuwa kasi ya Serikali ya kipindi hiki cha miaka mitano inahitaji mchango madhubuti wa sekta ya habari na mawasiliano na hilo haliwezi kufikiwa bila ya viongozi na watendaji wa Serikali na taasisi zake kutoa ushirikiano wa karibu na vyombo hivyo.

Sisi tunaamini kuwa kauli hii ya Mheshimiwa Rais ina ujumbe mzito kwa wahusika na kwamba ni imani yetu pia kuwa wataelewa kusudio la kauli hii. Inawezekana timiza wajibu wako.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akipokea maandamano ya Wafanyakazi mbali mbali wa Taasisi za Serikali na Binafsi,wakati wa sherehe za siku ya Wafanyakazi Duniani katika viwanja vya Ukumbi wa Salama, Hoteli ya Bwawani Mjini Unguja, tarehe 01 Mei, 2016*

# Sherehe za siku ya wafanyakazi - Mei Mosi

- Serikali imejidhatiti kuendelea kuimarisha maslahi ya wafanyakazi
- Shirikisho la vyama huru la wafanyakazi lapongeza juhudi za Serikali
- Vyasisitiza kuwa haki na wajibu ni watoto pacha

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (ZATUC) nchini kwa mara nyengine tena vimedhihirisha dhamira yao ya dhati katika kuimarisha mazingira ya kufanyakazi ikiwemo maslahi bora zaidi ya wafanyakazi, huku ikitilia mkazo suala la haki na wajibu kuwa ni watoto pacha.

Dhamira hiyo ya Serikali kwa kushirikiana na Shirikisho Vyama Huru vya Wafanyakazi imebainika wazi katika maadhimisho ya sherehe za siku ya wafanyakazi ampapo pande zote mbili zilibainisha mafanikio yaliyopatikana katika kuzipatia ufumbuzi changamoto mbali mbali ambazo zimekuwa zikiikabili sekta ya kazi na mipango ya baadae ya kuimarisha sekta hiyo.

Katika kufikia mafanikio ya utekelezaji wa dhamira hiyo, Serikali tayari imeshaweka utaratibu mzuri wa kisheria baina ya mwajiri na mwajiriwa kwa kuweka vyombo maalum vyenye uwezo wa kusikiliza, kushauri na kupendekeza maslahi ya wafanyakazi. Utaratibu wa aina hii ni mashuhuri duniani kote ili kuuthamini mchango wa wafanyakazi katika utoaji wa huduma kwa umma, kuchangia maendeleo na kudumisha amani, utulivu na usalama kwa lengo la kuimarisha huduma za jamii na utendaji katika sekta ya umma na sekta binafsi. Madhumuni makubwa ya utaratibu huu ni kuepusha migogoro na mifarakano katika sehemu za kazi.

Ni ukweli ulio wazi kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kuimarisha utaratibu wa majadiliano ya pamoja kazini ili kuimarisha uhusiano bora na kuondoa mizozo kwenye kazi, ili kuleta ufanisi. Serikali imehakikisha kwamba vyombo vyote vya majadiliano kati ya waajiri na waajiriwa vimeundwa na vinafanya kazi ipasavyo. Vyombo hivyo ni pamoja na Bodi ya Ushauri wa Mambo ya Kazi, Bodi ya Ushauri wa Mishahara, Kamati ya UTATU na Kamati ya Afya na Usalama Kazini. Vyombo vyote hivi vina uwakilishi wa wafanyakazi kupitia Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Zanzibar, Jumuiya ya




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akiwapungia mkono wafanyakazi kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais walioshiriki maandamano wakati wa sherehe za sikuya Wafanyakazi Duniani katika viwanja vya Ukumbi wa Salama, Hoteli ya Bwawani Mjini Unguja, tarehe 01 Mei, 2016*

Waajiri na Wajumbe kutoka Serikalini.

Hivi sasa tayari Serikali imekwishaunda chombo cha juu cha Kitaifa cha Majadiliano katika Sekta ya Umma na kimeshaanza kufanya vikao vyake kwa mujibu wa Sheria na kanuni zinazoongoza vikao hivyo. Hatua hii ni muhimu sana na hasa kwa vile Serikali itaendelea kuwashirikisha wafanyakazi katika mambo yanayowahusu. Itakuwa ni vyema basi iwapo wawakilishi wa wafanyakazi wanaoingia katika vyombo hivyo wataitumia ipasavyo fursa hiyo na kuwasilisha hoja zenye kuzingatia maslahi ya wafanyakazi na jamii yote kwa jumla.

Mfumo mzuri wa Sera, Sheria na Kanuni zinazohusiana na masuala ya kazi, ikiwemo Sheria Namba 11 ya mwaka 2005 na Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011 umekwishawekwa ili kuhakikisha kwamba kunakuwepo na utaratibu mzuri ambao unasimamia masuala ya kazi hapa nchini. Hivi sasa Serikali inaendelea na utekelezaji wa Sera ya Ajira ya mwaka 2009 na Kanuni za kazi ikiwemo Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014. Ni dhahiri kwamba, mashirikiano ya pamoja kati ya wafanyakazi, waajiri na Serikali ni suala muhimu katika kufanikisha utekelezaji mzuri na wenye tija wa sera, sheria na kanuni zinazohusiana na masuala ya kazi.

Akizungumza kwenye kilele cha sherehe za siku ya wafanyakazi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein aliwaahidi wafanyakazi kwamba Serikali itajitahidi kuchukua hatua katika kutimiza wajibu wake ili ifikie lengo la kupata ufanisi zaidi.

Alisema Serikali inatambua umuhimu wa kuandaa mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba afya za wafanyakazi zinalindwa dhidi ya maradhi au majanga yanayoweza kuwapata wafanyakazi wakiwa kazini au nje ya mazingira ya kazi. Katika kuikabili hali hiyo, katika kipindi hiki cha pili cha Awamu Saba, Serikali imeweka mkazo katika kuziimarisha huduma za afya na kuandaa utaratibu bora zaidi wa kutoa huduma hizo, pamoja na kukamilisha utaratibu wa kuanzisha Bima ya Afya kwa wafanyakazi wa Sekta ya Umma. Lengo la mipango hii ni kuwaondoshea wananchi na wafanyakazi mzigo wa gharama za matibabu wakati wanapougua.

Alitoa wito kwa waajiri wa sekta binafsi ambao bado hawajaanzisha huduma hizo na wao waanze kujipanga ili waweze kuwaingiza wafanyakazi wao katika utaratibu wa aina hii. Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuendeleza utaratibu wa kupima afya kila baada ya kipindi maalum na kufanya mazoezi kwa lengo la kukabiliana na maradhi mbali mbali.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, imeshaanza kazi katika kipindi chake cha pili ambapo mipango na vipaumbele vya Serikali katika kipindi hicho kwa sekta mbali mbali vilielezwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati alipokuwa akilizindua Baraza la Tisa la Wawakilishi, tarehe 05 Aprili, 2016.

Katika hotuba yake hiyo, alieleza wazi wazi azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya kuimarisha ukuaji wa mapato na kuziba mianya ya uvujaji wa mapato. Vile vile, Rais wa Zanzibar alisisitiza umuhimu wa kuzingatiwa kwa Sheria Namba 9 ya mwaka 2005 ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma pamoja na kuhakikisha ubora wa miradi na ununuzi wa vifaa na huduma mbali mbali unaofanywa kwa kuzingatia thamani ya fedha zinazotumika.



*Baadhi ya Viongozi na Wafanyakazi wa Taasisi mbali mbali za Serikali na Binafsi wakiwa katika sherehe za siku ya Wafanyakazi Duniani katika Ukumbi wa Salama, Hoteli ya Bwawani Mjini Unguja, tarehe 01 Mei, 2016*

Ili kuthibitisha dhamira ya kweli ya Serikali katika suala la uwajibikaji, Dk. Shein alirejea kauli yake mbele ya wafanyakazi hao kwa kusema kuwa Serikali itayasimamia mambo ya msingi kwa vitendo. Aidha, Serikali itapambana na vitendo vyote vya rushwa na uhujumu wa mali ya umma, ubadhirifu, uzembe, uonevu na dhulma na kwamba watakaobainika kujiingiza na kufanya vitendo hivi, watachukuliwa hatua kwa kuzingatia sheria na misingi ya utawala bora bila ya kumdhulumu mtu yoyote.

"Wakati tulionao si wakati wa maneno, sasa ni wakati wa vitendo. Jukumu letu ni kuipeleka mbele nchi yetu ili ifikie nchi yenye uchumi wa kati. Kwa hivyo, lazima sote tujitahidi kuongeza kasi katika kujituma na kufanya kazi za halali. Tuwe wabunifu na tujisimamie wenyewe badala ya kusubiri kusimamiwa na kuelekezwa hata katika yale mambo ambayo yamo ndani ya uwezo wetu", alisisitiza Mhe. Rais wa Zanzibar katika hotuba yake kwenye sherehe za siku ya wafanyakazi – Mei Mosi.

Alielezea matumaini yake kwamba Zanzibar tunao uwezo wa kupiga hatua kubwa zaidi ya maendeleo na kwa haraka, iwapo tutatumia vyema maarifa tuliyonayo, rasilimali alizotujaalia Mwenyezi Mungu na uzoefu tulioupata katika kipindi cha miaka 52 sasa, tangu yalipofanyika Mapinduzi Matukufu ya Januari 12, mwaka 1964.

Serikali imekwishaandaa utekelezaji wa mipango mikuu ya maendeleo ambayo wajibu wa wafanyakazi na wananchi wote ni kushirikiana na Serikali katika kuitekeleza mipango hiyo kwa manufaa ya watu wote bila ya kujali aina yoyote ya ubaguzi. Ushiriki wa wafanyakazi wa sekta mbali mbali za umma na sekta binafsi ni tegemeo la Serikali katika kuufanikisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ili kupata mafanikio katika kukuza uchumi wa taifa na kuimarisha huduma za jamii.


Mafanikio ya haraka yanaweza kupatikana katika utekelezaji wa mipango hiyo iwapo wafanyakazi kwa pamoja watatimiza wajibu wao kwa moyo wa uzalendo huku wakizingatia umuhimu wa kuendeleza amani, umoja na mshikamano mambo ambayo ndiyo msingi wa mafanikio yaliyokwishapatikana.

Ili kuweza kupata mafanikio yaliyokusudiwa, viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi vya hapa Zanzibar nao hawana budi kuendelea kujidhatiti katika kutimiza wajibu wao kwa kuwakumbusha na kuwataka wafanyakazi watimize wajibu wao. Wafanyakazi watakiwe kuzingatia nidhamu kazini na maadili ya kazi ili ipatikane tija kwenye kazi na matokeo mazuri kwa ustawi wa wananchi wote. Wafanyakazi ni lazima wawajibike kwa mujibu wa majukumu yao na kwa kuzingatia Sheria Namba 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 na kanuni zake.

Kuhusu tatizo la ajira, Zanzibar kama zilivyo nchi nyengine zinazoendelea na zile zilizoendelea, nayo inakabiliwa na tatizo la ukosefu wa ajira za kutosha kwa wananchi na hasa kwa vijana. Hata hivyo, Serikali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, iliongeza nafasi za ajira 5,370 katika taasisi mbali mbali Serikalini ili kupunguza tatizo la ajira. Aidha, Sekta Binafsi ilitoa nafasi za ajira 25,006 zikijumuisha ajira za nje ya nchi. Hii ni hatua kubwa ingawa bado nafasi hizo zilizopatikana ni chache sana na bado suala la ajira linaendelea kuwa ni changamoto kubwa nchini. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbali mbali katika kukabiliana na changamoto hiyo kwa kushirikiana na sekta binafsi.

# Risala ya kuukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani mwaka 1437 - Hijria sawa na mwaka, 2016 Miladia

## Risala ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Alhaj Dk. Ali Mohamed Shein ya kuukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani mwaka 1437 - Hijria sawa na mwaka, 2016 Miladia 5 Juni, 2016



***Alhajj Dk. Ali Mohamed Shein***
***Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi***

BISMILLAHI RAHMAN RAHIM,

Naanza kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema zote ndogo ndogo.

**Ndugu Wananchi,**
Assalamu Aleikum Warahmatullahi Wabarakatuhu.

Ni wajibu wetu kumshukuru Mola wetu (SW) kwa kutujaalia neema ya uhai na leo hii tukajaaliwa kuukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu aliyelijaaliya jua kuwa na mwangaza, na mwezi ukawa na nuru, na akaupimia vituo ili tujue idadi ya miaka na hisabu yake. Tunamuomba atujaaliye siha, nguvu na uwezo kwa kuitekeleza ibada ya Saumu katika mwaka huu 1437 Hijria, kwa unyenyekevu, utiifu na katika hali ya amani na utulivu.

Tunamshukuru Mola wetu kwa kutuwezesha kujuumuika na waislamu wenzetu katika nchi mbali mbali leo hii katika kuukaribisha mwezi huu mtukufu. Ni neema na hidaya kubwa kwetu tukizingatia kuwa wako wenzetu tuliofunga nao Ramadhani iliyopita, na leo hii hatunao tena, wametangulia mbele ya haki. Tunamuomba Mwenyezi Mungu uwasamehe makosa yao na awape makaazi mema Peponi wale wote waliotangulia mbele ya haki. Amin.

**Ndugu Wananchi,**

Wakati tunaukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ni vyema tukakumbushana baadhi ya mambo muhimu yanayopendeza kufanywa katika mwezi huu.

Huu ni Mwezi Mtukufu ambao ndani yake imeteremshwa Qur'ani kama alivyotubainishia Subahana Wataala katika Kitabu chake kitukufu cha Qur'ani katika aya ya 185 ya Suratul Baqara, kwa kusema:

"Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa ndani yake Qur-an kuwa ni uongofu kwa watu, na hoja zilizowazi za uwongofu na upambanuzi .. … … … …" (2:185)

Ilivyokuwa katika mwezi huu ndio Qur'ani iliteremshwa kwa Mtume wetu Muhammad (SAW), tuna wajibu wa kufanya bidii katika kuisoma na kuifahamu Qur'an, ili tuweze kuishi kama Mwenyezi Mungu alivyotuelekeza na tupate baraka zake hapa duniani na kesho mbele ya haki.

Vile vile, hatuna budi kuhimizana katika kuzitekeleza Sala za Fardhi na kusali Sala za Sunna mbali mbali hasa katika nyakati za usiku. Huu ni mwezi, ambao ndani yake unapatikana usiku wenye heshima kubwa (Laylatul Qadr) ambao ibada ya usiku huo imebarikiwa kuliko ibada ya miezi elfu moja, na kwa hekima yake, Allah (SW), hakutubainishia kuwa ni usiku wa tarehe ngapi.

Bwana Mtume Muhammad (SAW) amesema: "Mwenye kusimama usiku wa Ramadhani kwa kufanya ibada hali ya kuwa na imani na kutaraji thawabu, anasamehewa mtu huyo, yote yaliyotangulia miongoni mwa makosa yake." (Bukhari na Muslim).

**Ndugu Wananchi,**

Vile vile, ni muhimu katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani tukakumbushana kuwa miongoni mwa ibada tukufu alizokuwa akizifanya Bwana Mtume (SAW) ni kutoa sadaka na alilipa umuhimu sana jambo hili hadi wakati wa kuondoka kwake duniani. Wakati Bwana Mtume Muhammad (S.A.W) alipokuwa katika sakaratul mauti kila alipopata fahamu alikuwa akimuuliza Bibi Aisha ('Radhiyallahu Unha) iwapo ameshazitoa sadaka zile dirhamu nne zilizokuwa nyumbani kwake wakati huo.

Kadhalika, kutoa kwake sadaka kulikuwa kukiongezeka katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Ni wajibu wetu tuishi, yeye akiwa ni mfano wa umma huu. Vile vile, tufanye bidii na kumtaja Allah, tufanye istighfari na kukaa Itikafu, tuharakishe kufungua wakati unapofika na tutekeleze sunna ya kula daku. Mambo haya yote yamepewa uzito mkubwa katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Tumuombe Allah atupe nguvu na uwezo wa kuyatekeleza mambo haya.

**Ndugu Wananchi,**

Sambamba na kuongeza juhudi katika kufanya mambo mema, ni wajibu wetu tuongeze juhudi katika kujizuwia ili tusifanye mambo maovu yaliyokatazwa ambayo yanaweza kubatilisha funga zetu au kufanya mambo ambayo hayapendezi kufanywa na mtu aliyefunga na yanayoweza kupunguza uzito wa mizani ya thawabu katika ibada zetu.

Wakati tunajiandaa na kufunga, ni muhimu sote tukafahamu kwamba hivi sasa teknolojia imevisogeza vishawishi vingi vinavyoweza kuibatilisha saumu karibu na nafsi zetu. Miongoni mwa vishawishi hivyo ni mitandao ya simu na intaneti.

Nimeona nikukumbusheni ndugu wananchi, kuhusu suala hili, kwa sababu nahisi bado tunachangamoto mbali mbali za kijamii na kidini zinazoibuka kutokana na matumizi mabaya ya mitandao. Bila ya kujijua, mtu anaweza kujikuta anafanya makosa pale anapoangalia mitandao yenye mambo yasiyopendeza, hasa katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Simu zimerahisisha mawasiliano katika jamii yetu, lakini vijana wetu wa kike na wa kiume, hufanya mazungumzo ya faragha yasiyoruhusiwa kidini baina ya vijana hao. Ni wajibu wetu waislamu tujiepushe na vitendo vinavyoweza kubatilisha saumu zetu kwa njia ya mitandao ya simu na kompyuta.

Wito wangu kwa mashekhe ni kwamba waendelee kutoa taaluma juu ya umuhimu wa matumizi bora ya mitandao na kwa pamoja tuhimizane juu ya umuhimu wa kuunga mkono juhudi zetu zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kushajihisha matumizi bora ya mitandao ya simu na kompyuta kwa kutumia mitandao ya intaneti.

**Ndugu Wananchi,**

Ni muhimu tukazingatia kuwa wakati tunaukaribisha Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani bado tumekabiliwa na tatizo la kuwepo kwa miripuko ya maradhi ya kipindupindu katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba. Hadi leo ambapo tunaukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani bado wapo wagonjwa wanaohudumiwa katika vituo vinavyotolewa utibabu wa maradhi ya kipundupindu, Unguja na Pemba.

Hali ya maradhi hayo yalipofikia hivi sasa ni nafuu sana, ikilinganishwa na kipindi cha wiki iliyoanzia tarehe 16 hadi 22 Aprili, 2016 ambapo wagonjwa wa kipindupindu walifikia 250 kwa Unguja na Pemba ndani ya wiki moja. Tunapaswa tuyadhibiti maradhi hayo kwa juhudi zetu zote.

**Ndugu Wananchi,**

Katika kuendeleza jitihada na mikakati ya kuyanusuru maisha ya wananchi na kujikinga na miripuko ya kasi ambayo inaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa harakati za maisha yetu na mwenendo mzima wa uchumi, Serikali itaendelea kuchukua tahadhari kwa kuchukua hatua mbali mbali kama zilivyotangazwa na Wizara ya Afya.

Serikali inajuwa kwamba uamuzi huu uliochukuliwa unaweza kuathiri utamaduni wetu wa kuandaa hafla na tafrija za kufutarisha zinazoandaliwa na wananchi, taasisi mbali mbali za Serikali na sekta binafsi katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Imani yangu ni kuwa, sote tutaendelea kushirikiana katika kuendelea kulitekeleza agizo hilo la Serikali, lengo letu liwe ni

kushirikiana katika kuyanusuru maisha yetu kwa kuyatokomeza maradhi haya kwa haraka zaidi ili tuweze kuendesha shughuli na harakati za maisha katika hali ya kawaida.

Nasaha zangu kwenu wananchi ni kuwa tuendelee kufuata miongozo ya usafi iliyotolewa na wataalamu wa afya na Serikali inaendelea kufanya tathmini kuhusu hali hiyo na itawapa taarifa kwa kadri hali inavyoendelea kuimarika.

**Ndugu Wananchi,**

Ni muhimu tukakumbushana kuwa Bwana Mtume Muhammad (S.AW) alikuwa akizidisha ukarimu katika mwezi huu wa Ramadhani. Siku zote alikuwa mkarimu, lakini alikuwa mkarimu zaidi katika mwezi huo. Kwa hivyo, ni wajibu wetu kufuata nyendo za Kiongozi wetu kwa kuzidisha ukarimu baina yetu katika Mwezi Mtukufu tunaouanza kesho.

Inasikitisha kuona kuwa, licha ya kuwa uislamu unahimiza kuoneana huruma, lakini wapo wafanyabiashara ambao huchukua fursa ya kupandisha bei bidhaa zao katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan, hasa zile bidhaa za chakula muhimu ambazo Serikali hupunguza ushuru ili kuwapa afueni wananchi. Nafahamu malalamiko yaliyopo hivi sasa, ambapo wafanyabiashara walipandisha bei za bidhaa kwa kisingizio cha uchaguzi. Hadi leo hii bei za bidhaa hizo bado ziko juu.

Serikali itaongeza juhudi za kuwafuatilia wafanyabiashara wenye tabia hiyo ya kupandisha bei za bidhaa muhimu bila ya sababu za msingi, jambo ambalo linaathiri hatua ya Serikali ya Mapinduzi ya kutoa unafuu wa ushuru wa bidhaa muhimu kwa wafanyabiashara, ili waziuze bidhaa hizo kwa wananchi kwa bei nafuu. Kadhalika, upandishaji wa bei usio na msingi unakwenda kinyume na malengo yetu ya kuanzishwa kwa biashara huru yenye ushindani. Serikali itaendelea kushirikiana na wafanyabiashara na itahakikisha kuwa bidhaa zote muhimu zinazohitajika na kutumika zaidi katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani zinapatikana wakati wote na bila ya usumbufu wowote.

**Ndugu Wananchi,**

Miongoni mwa mambo muhimu kwa waislamu ni kuimarisha umoja na mshikamano miongoni mwetu. Mtume Muhammad (S.A.W) katika maisha yake amehimiza sana suala la kuvumiliana, kupendana na kustahamiliana na kuishi bila ya kukhitilafiana kwa mambo madogo madogo.

Kadhalika, Mtume Muhammad (SAW) ametufundisha umuhimu wa kudumisha umoja na udugu kwa kutwambia: "Msikate ujamaa, msigeuke, msichukiane na msihusudiane. Nyinyi mkiwa ni waja wa Mwenyezi Mungu, dumisheni udugu. Ndugu wawili wasinuniane kwa zaidi ya siku tatu" (Imepokewa na Imam Malik).

Katika hadithi nyengine Mtume Muhammad (S.A.W) anatufundisha kwamba:

"Tabasamu unayoonesha kwa nduguyo ni sadaka" (Tirmidh).

Qur-ani Tukufu, inahimiza suala la kukuza udugu kwa kutwambia katika aya ya 10 ya Surat al-Hujurat

"Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu basi patanisheni baina ya ndugu zenu na mcheni Mwenyezi Mungu ..." (49:10).

Kutokana na mafundisho hayo ya Qur'ani na Hadithi za Mtume wetu Muhammad (S.A.W) ni wajibu wetu wa kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa anafanya vitendo vyema, anaepuka chuki na hasama na kuimarisha mapenzi miongoni mwa Wazanzibari wote. Tuimarishe mshikamano wetu katika kulinda amani ili tuweze kuitekeleza saumu na ibada nyengine katika hali ya amani na utulivu, tukitambua kuwa amani ndio msingi unaotuwezesha na kutupa uhuru wa kufanya ibada kwa utulivu na kutafuta riziki za halali kwa familia zetu.

Ni wajibu wetu kumshukuru Mwenyezi Mungu Muweza kwa kuiweka nchi yetu katika hali ya amani na salama na sote tunafahamu kuwa sisi ni wamoja na kwa hivyo, chuki na husda hazina tija wala hazina nafasi katika kuijenga Zanzibar ya leo.

Napenda nikuhakikishieni ndugu wananchi kuwa, Serikali zetu mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya amani na salama.

**Ndugu Wananchi**,

Nafahamu kwamba licha ya jitihada mbali mbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuwapatia wananchi huduma bora za jamii, lakini bado huduma hizo hazipatikani vizuri katika baadhi ya maeneo. Kwa mfano, bado shida ya maji safi na salama inaendelea kuwakumba wananchi katika baadhi ya maeneo.

Kwa hivyo, katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, bado wananchi wanaoishi katika maeneo hayo wanaweza kupata shida ya ukosefu wa maji.

Kutokana na hali hiyo, kwa mara nyengine ninaiagiza Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na Mamlaka ya Maji ya Zanzibar (ZAWA) ifanye kila jitihada ili iwapatie wananchi maji safi na salama, kwa kutumia magari katika sehemu zote ambazo zina upungufu wa maji safi na salama. Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA ahakikishe kwamba kazi hii ya kuwapatia wananchi maji inafanyika kwa mafanikio makubwa. Natoa wito kwa wananchi washirikiane na Mamlaka hiyo ili waifanikishe shughuli hiyo ipasavyo.

**Ndugu Wananchi,**

Napenda nimalizie risala yangu kwa kukutakieni nyote kheri, rehema na baraka za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Namuomba Mwenyezi Mungu atuzidishe mapenzi baina yetu na aizidishe baraka na neema katika nchi yetu.

Ramadhani Njema.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipiga mpira kuashiria ufunguzi wa Mashindano ya Tamasha la Michezo ya Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu Zanzibar yaliyofanyika katika Uwanja wa Amaan Mjini Unguja, tarehe 21 Mei, 2016*

# Dk. Shein amewasisitiza wazazi, walezi umuhimu wa michezo maskulini

Utafiti wa kisayansi na zoefu wa muda mrefu umeonesha kuwa michezo kwa jumla siyo tu inaimarisha afya za wanamichezo, lakini ni shughuli inayoimarisha ufahamu wa wanafunzi maskulini na vipaji vya uongozi bora huanza kuonekana katika miaka ya mwanzo wakati wanafunzi wakiwa skuli. Kumbukumbu zinaonesha kuwa wengi miongoni mwa viongozi maarufu duniani, walianza kuonekana vipaji vyao wakiwa skuli ama kwenye michezo au kwenye harakati za uongozi wa skuli.

Kuna mifano mingi ya viongozi wazuri walioshiriki michezo tokea wakiwa wanafunzi na uongozi wao katika utumishi wa umma umekuwa wa kupigiwa mfano. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ni mmoja kati ya mifano ya viongozi wa aina hiyo. Katika maisha yake ya skuli, yeye alikuwa ni mwanamichezo mahiri aliyeshiriki michezo mingi bila ya masomo yake kuathirika. Michezo ilimpelekea hadi kufikia kuwa kocha wa mpira wa miguu aliyepata sifa kubwa.

Katika hili, hatuwezi kuacha kumzungumzia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, ambaye kwa wakati wake alikuwa mwanasoka na pia mwanariadha maarufu aliyeweka rikodi ya mita 100, ambayo inasemekana kuwa hadi leo haijapata kuvunjwa hapa Zanzibar. Aidha, Dk. Shein kutokana na kipaji chake cha uongozi, Rais wa kwanza wa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Karume, alimteua kuongoza timu ya wanafunzi kadhaa waliokuwa wanakwenda kusoma nchini Urusi mwaka 1969. Hivyo, uamuzi wa Dk. Shein wa kuhamasisha kurejeshwa vuguvugu la michezo katika skuli mbali mbali, haukuja kwa bahati mbaya, bali ni dhamira yake ya kweli akijua kwa uhakika tija inayopatikana kutokana na michezo hiyo.

Katika kuendeleza azma yake ya kuibua vipaji vya michezo kwa watoto, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein amekuwa akiwahamasisha wazazi na walezi kuwaruhusu watoto wao kushiriki katika michezo mbali mbali na kuondokana na dhana potofu ambayo imejengeka miongoni mwa baadhi ya wazazi na walezi katika jamii kwamba ushiriki wa watoto katika michezo mbali mbali maskulini unasababisha wanafunzi kupoteza muda wao wa masomo na hivyo kupelekea kufanya vibaya kwenye masomo yao.

Dhana nyengine ambayo vile vile siyo sahihi, inajengwa na baadhi ya wazazi na walezi kwamba kitendo cha wanafunzi kupewa uongozi kuongoza



***Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwapungia mkono wanamichezo wa Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu Zanzibar wakati wa ufunguzi wa Mashindano ya Tamasha la Michezo ya Vyuo hivyo yaliyofanyika katika Uwanja wa Amaan Mjini Unguja, tarehe 21 Mei 2016. Kushoto ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mheshimiwa Riziki Pembe Juma***

madarasa yao kinawanyima watoto wao fursa ya kusoma na hivyo kufanya vibaya katika mitihani yao ikilinganishwa na wanafunzi wenzao ambao hawakupewa majukumu hayo.

Akizindua mashindano ya michezo ya Shirikisho la Michezo ya Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu Zanzibar (ZAHILFE) tarehe 21 Mei, 2016 katika Uwanja wa Amaan, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alibainisha wazi umuhimu wa michezo katika jamii, maskuli na taasisi za elimu kwa jumla. Alisema michezo ni nyenzo muhimu ya kujenga umoja, maelewano na mshikamano kwa wanavyuo, wanafunzi wa skuli na jamii kwa jumla.

Katika kuelezea umuhimu wa michezo kwa kuzingatia mabadiliko ya dunia kisiasa, kijamii na kiuchumi, Dk. Shein alisema, "Michezo hivi sasa imepata kipaumbele kikubwa kwani mbali ya kuwa na dhima kuu ya uburudishaji, lakini vile vile inatoa ajira kwa vijana ndani na nje ya nchi". Aliendelea, "Hivi sasa vijana wengi wa Kitanzania tayari wamepata ajira kucheza soka la kulipwa nje ya nchi."

Dk. Shein alisisitiza kuwa katika taasisi za elimu, michezo ina mchango muhimu wa kuimarisha nidhamu za wanafunzi katika masomo yao na kuwapelekea kupata matokeo mazuri. Aidha, nidhamu hiyo huwajengea kuwa na mahusiano mema wenyewe kwa wenyewe na jamii inayowazunguka.

Kihistoria, michezo katika taasisi za elimu hapa nchini sio jambo jipya kwani tangu kupatikana kwa uhuru wa Zanzibar baada ya kufuzu kwa Mapinduzi Matukufu ya Januari 12, mwaka 1964, tumeshuhudia kuanzishwa kwa Wizara ya Elimu, Mila na Utamaduni yenye jukumu muhimu la kushughulikia masuala ya michezo katika skuli na taasisi zote za elimu.

Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein, jitihada maalumu za kuchochea vuguvugu la michezo katika maskuli na taasisi za elimu ya juu zimechukuliwa. Katika kufanikisha azma hiyo ya Serikali, Dk. Shein, aliamua kuanzisha Idara mpya ya Michezo na Utamaduni katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili kuoanisha masuala ya michezo na elimu. Matokeo ya jitihada hizo yameanza kuonekana kwa kurudi kwa hamasa za michezo katika Tamasha la Elimu bila ya malipo ifikapo mwezi Septemba kila mwaka.

Katika hatua nyengine, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Saba, katika kipindi hiki cha Awamu ya Pili imewahakikishia wananchi wote wa Zanzibar kuwa itayaendeleza kwa vitendo mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya michezo. Vile vile, itaimarisha mashindano ya riadha ya Wilaya na kuliimarisha Bonanza la Michezo na vikundi vya mazoezi linalofanyika kila tarehe Mosi Januari ya kila mwaka. Aidha, Serikali itaongeza juhudi katika kuimarisha michezo maskulini na vyuo vya elimu ya juu ambapo kipindi hiki Serikali inadhamiria kufundisha somo la michezo katika Skuli teule sita (6) za Sekondari Unguja (4) na Pemba (2).

Kadhalika, Serikali itakamilisha matengenezo ya Kiwanja cha Mao Tse Tung na kujenga viwanja vya michezo kila Wilaya. Hata hivyo, Serikali kwa kushirikiana na wananchi itazidi kuhamasisha michezo ya asili ya Zanzibar, ikiwemo mashindano ya



***Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na mchezaji wa Timu ya Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar wakati alipokuwa akiikagua timu hiyo wakati wa ufunguzi wa Mashindano ya Tamasha la Michezo ya Vyuo hivyo yaliyofanyika katika Uwanja wa Amaan Mjini Unguja, tarehe 21 Mei, 2016***

Resi za Ngalawa, Bao, Karata, Mchezo wa Ng'ombe na kadhalika. Kwa hivyo, Serikali inatoa wito kwa makundi mbali mbali katika jamii wakiwemo watu wenye mahitaji maalum kushiriki katika michezo na vile vile Serikali inatarajia kuvipatia vifaa vyama vya michezo vinavyohusika ili viweze kushiriki kikamilifu katika kuendeleza michezo nchini.

Tunaipongeza kwa dhati kabisa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa jitihada zake katika kuwaunganisha na kuwaweka pamoja wanafunzi wote wa Shirikisho la Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu hapa Zanzibar. Tuna imani kuwa, Zanzibar ina uwezo wa kupata wanamichezo bora watakaoweza kuendelezwa na hatimae kupata wachezaji mahiri wa michezo mbali mbali, watakaoiletea sifa nchi yetu katika medani za kimataifa. Hivyo, walimu na wanamichezo, waamuzi na makocha wahakikishe kuwa mashindano na michezo inaendeshwa kwa kuzingatia sheria za michezo za kimataifa ikiwa vile vile ni maandalizi kwa timu zetu zinazotuwakilisha.

Wakati akizindua michezo ya Shirikisho la Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu, Dk. Shein aliukumbusha uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufanya maandalizi mazuri ya timu za Zanzibar zilizotarajiwa kushiriki katika mashindano ya Umoja wa Michezo ya Skuli za Sekondari Tanzania (UMISSETA) ili kwenda kushinda na sio kushiriki tu. Michezo ya UMISSETA ilipangwa kufanyika katika viwanja vya Chuo cha Ualimu Butimba Mwanza kuanzia tarehe 13 Juni hadi tarehe 24 Juni, 2016. Hata hivyo, mashindano hayo yaliahirishwa hadi itakapotajwa tarehe nyengine.

Kwa mara ya kwanza katika michezo hiyo, Zanzibar ilipangwa kuwa na timu za Kanda ya Unguja na Kanda ya Pemba, ili kutoa ushiriki mpana wa timu za Zanzibar. Kanda ya Unguja ilikuwa na timu ya mpira wa miguu wanaume, mpira wa wavu na mikono wanaume, riadha wanaume na sanaa na mpira wa meza wanawake na wanaume. Vile vile, kulikuwa na mshiriki mmoja wa mchezo wa bao.

Akizungumza na jarida la Ikulu, Mkurugenzi wa Idara ya Michezo na Utamaduni; Maalim Hassan Hairallah alisema Kanda ya Pemba itakuwa na timu ya mpira wa miguu, mpira wa wavu na mpira wa vikapu kwa wanaume. Aidha, kutakua na timu za mpira wa meza na riadha kwa wanawake na wanaume.

Mkurugenzi huyo amesema kuwa ameridhishwa na maandalizi ya timu zote zilizopangwa kuiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya mwaka huu na amewashukuru wazazi, walimu na makocha wa timu hizo kwa mchango wao katika kufanikisha ushiriki wa timu za Zanzibar yaliyokuwa yamepangwa kufanyika Butimba Mkoani Mwanza. Aidha, kwa uzito maalum alietoa shukurani za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuzipatia timu hizo vifaa vya michezo. Vifaa hivyo, vilikabidhiwa tarehe 05 Juni, 2016 na Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Nd. Omar Hassan Omar kwa niaba ya Mhe. Rais.

Lengo la Dk. Shein la kutaka kuirejesha hadhi ya Zanzibar katika tasnia ya michezo lazima iungwe mkono na wapenzi wote wa michezo kwa kuwa tayari kutoa michango yao ya hali na mali. Wahenga walisema "Kidole kimoja, hakivunji chawa". Huu ni wajibu wetu sote na tuwe na imani kuwa uwezo wa kupiga hatua kubwa zaidi katika kuimarisha michezo nchini tunao.

Taasisi za Serikali, taasisi binafsi, wafanya biashara, vikundi na watu mmoja mmoja tuoneshe uzalendo na mapenzi yetu katika kuchangia kuimarisha sekta ya michezo hapa Zanzibar kwa kuzingatia umuhimu wake katika jamii na kuirudisha hadhi ya nchi yetu kitaifa na kimataifa katika tasnia ya michezo. Tuzingatie wajibu wa kila mmoja wetu kwa mujibu wa Sera ya Michezo ya Zanzibar ya mwaka 2007 jambo ambalo ni kuunga mkono dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Saba chini ya Dk. Shein katika kuimarisha sekta ya michezo, Zanzibar.

# Dk. Shein azungumza na wana-habari wa SMZ



***Baadhi ya Waandishi wa Habari wa vyombo vya Serikali wakimsikiliza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alipokuwa akizungumza nao pamoja na Viongozi wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo katika ukumbi wa Ikulu Mjini Unguja, tarehe 09 Juni 2016***

Lilikuwa ni tukio la kwanza la aina yake kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kukutana na kuzungumza ana kwa ana na wanahabari kutoka vyombo vya habari vya Serikali kuzungumzia/kujadili mustakabala wa taaluma yao na wao wenyewe, kama walivyokiri baadhi ya watumishi wakongwe wa vyombo hivyo walioanza kufanya kazi tokea Awamu ya Kwanza ya uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa wengi wa watumishi hao, ni mkutano utakaobaki katika kumbukumbu zao kwa miaka mingi ya utumishi wao serikalini kwa kupata fursa hiyo adhimu ya kubadilishana mawazo na Mheshimiwa Rais.

Chimbuko la mkutano huo ni ombi lililowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais na watumishi wa vyombo hivyo wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari alipokuwa akitangaza Baraza la Mapinduzi Aprili 9, 2016.

Kwa upande mmoja mkutano huu ulimpa fursa Mheshimiwa Rais kuwafahamu kwa karibu zaidi watumishi wa vyombo hivi vya serikali ambavyo kama alivyoeleza mwenyewe kuwa vimekuwa vikifanyakazi nzuri katika kuteleleza majukumu yake ya kila siku.

Ilikuwa ni fursa pia kwa Mheshimiwa Rais kujifunza kutoka kwa watumishi hao uzoefu wao na mazingira yao ya kazi ikiwemo changamoto wanazokabiliana nazo kila siku.

Kwa watumishi hao ilikuwa ni fursa ya pekee kuzungumza na Mheshimiwa Rais kueleza mazingira yao ya kazi na kutoa ushauri wao kwa serikali kuhusu namna bora zaidi ya kuimarisha vyombo hivyo.

Kwa hakika ulikuwa mkutano muhimu na pengine inaweza kusemwa kuwa ulichelewa kufanyika kutokana na uzoefu uliopatikana katika kubadilishana mawazo kati ya Mheshimiwa Rais na watumishi hao.

Ni jambo la kufurahisha kuona watumishi wa vyombo hivyo vya habari vya serikali walionesha ukomavu mkubwa katika kujadili masuala mbalimbali ya taasisi zao na kutoa ushauri ambapo serikali kupitia uongozi wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo uliahidi kuufanyia kazi.

Katika mkutano huo watumishi hao walieleza changamoto mbalimbali zinazowakabili katika kutekeleza majukumu yao ikiwemo upungufu wa vitendea kazi pamoja na suala la maslahi ambalo kama watumishi wengine wa serikali hicho ndio kilio chao.

Jambo la kutia moyo ni kuwa uongozi mpya wa Wizara hiyo ambao uliteuliwa mara baada ya uchaguzi mkuu wa marudio wa tarehe 20 Machi, 2016 umeanza kuzifanyia kazi baadhi ya changamoto hizo.

Tungependa kurejea pongezi na shukrani za Mheshimiwa Rais kwa uongozi wa wizara kwa kukutana na wafanyakazi wa taasisi zilizo chini yao vikiwemo vyombo vya habari vya serikali na kuzungumza nao ili kufahamu vyema mafanikio yao na changamoto zinazowakabili katika mazingira yao ya utendaji kazi.

Mikutano kama hiyo ni muhimu na inapaswa kufanyika mara kwa mara katika kila wizara na idara za serikali ili kuhakikisha kuwa wizara na taasisi zake zinafikia malengo yaliyowekwa katika kuwatumikia wananchi.

Kitendo cha Mheshimiwa Rais kukubali ombi la kukutana na watumishi




***Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Waandishi wa Habari wa vyombo vya Serikali pamoja na Viongozi wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo katika ukumbi wa Ikulu Mjini Unguja, tarehe 09 Juni, 2016***

wa vyombo hivyo vya habari vya serikali, ni uthibitisho mwingine wa usikivu wa Mheshimiwa Rais na serikali yake.

Ni kitendo kinachoonesha utayari wa Mheshimiwa Rais kusikiliza na kutenda kwa manufaa ya wananchi na Zanzibar kwa ujumla wake. Dk. Shein tangu kuingia madarakani ameonesha kwa vitendo utayari wake kushirikiana na wananchi katika kusukuma mbele maendeleo ya nchi.

Si mara ya kwanza au ya pili kuitikia mwaliko au ombi la wananchi kuwatembelea au kuonana nao kama alivyofanya kwa watumishi hawa wa vyombo vya habari vya serikali.

Dk. Shein ameahidi kuwa huo hautakuwa mkutano wake wa mwisho wa ana kwa ana na watumishi hao na kwa kudhihirisha uungwana na utayari wake alikubali tena ombi la kufanya ziara katika kila chombo cha habari kwa nyakati tofauti ili kujionea hali halisi ya vyombo hivyo.

Kwa hivyo ni jukumu la kila kiongozi katika serikali kuiga mfano wa Mheshimiwa Rais kwa kukutana na watumishi na wananchi na kusikiliza hoja na maoni yao pamoja na kuchukua hatua zinazopaswa kuchukuliwa pasi na kusubiri.

Kama alivyoeleza mwenyewe katika mkutano huo kuwa katika utumishi na uongozi, mawasiliano ni muhimu iwe sehemu za kazi au hata katika maeneo ya makazi kwa kuwa huko nako kuna wananchi ambao wanayo mengi ya kuzungumza na kuelimishana na viongozi wao.

Alitolea mfano wa vikao na mikutano kama hiyo kuwa njia mojawapo ya mawasiliano ambayo kwa upande mmoja yanajenga mahusiano mema kati ya viongozi na wanaoongozwa na kwa upande wa pili njia hiyo inajenga mazingira mazuri ya utendaji kazi ambayo ni moja ya misingi ya kufikia malengo yaliyowekwa katika sehemu za kazi.

Katika mnasaba huo, alitoa wito kwa viongozi wa taasisi zikiwemo za habari kuitisha vikao vya mara kwa mara kujadili masuala mbalimbali yanayohusu taasisi zao ili kurahisisha utendaji kazi na kuleta ufanisi ili hatimae kuziwezesha taasisi kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Lakini kwa upande wa vyombo vya habari vya serikali alivikumbusha tena wajibu wake kwa jamii ambao ni kuhabarisha, kuelimisha, kuhamasisha na kuburudisha kazi ambayo amesema si haba kwa kuwa vyombo hivyo vimekuwa vikijitahidi kuutekeleza pamoja na kukabiliwa na changamoto kadha wa kadha.

Dk. Shein aliwaeleza watumishi hao kuwa vyombo vya habari vya serikali vimekuwa njia kuu ya kuwapasha habari wananchi hivyo hawana budi kuifanya kazi yao kwa weledi mkubwa na kufuata maadili, sera na maagizo ya serikali.

Alibainisha kuwa kumefanyika uwekezaji mkubwa katika ZBC TV hivyo serikali na wananchi wangependa kuona mabadiliko makubwa katika upatikanaji wa matangazo na ubora vipindi vyake ili taasisi hiyo iendelee na sifa na ubora uliozoeleka na watazamaji wake.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Rais aliahidi kuhakikisha changamoto zinazovikabili vyombo hivyo vya habari vya serikali zinatafutiwa ufumbuzi hatua kwa hatua kwa kushirikiana na uongozi wa wizara husika.



*Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akiwa amenyanyua mikono kuitikia dua pamoja na watoto na wanafamilia ambazo zimeathiriwa na mafuriko wakati alipofika kuwafariji na kuwapatia misaada mbali mbali katika kambi yao Skuli ya Mwanakwerekwe C Wilaya ya Magharibi B Unguja, tarehe 03 Mei, 2016*

# Tahadhari ichukuliwe kujiepusha na maafa – Mama Mwanamwema

Maafa ni matukio ambayo hutokea bila ya kutarajiwa, na wengi wanaamini kwamba ni matukio yanayotokana na shani yake Mwenyezi Mungu. Imani hii inapata nguvu zaidi kutokana na daraja kubwa isiyo na kifani aliyonayo Muumba ya kujua asichokijua binadamu yoyote.

Licha ya wanasayansi kujaribu kubainisha baadhi ya mambo ambayo zamani yalionekana kuwa ni miujiza, bado mambo mengi yamebaki kuwa mtihani mkubwa kwao na kumuachia mwenyewe Mwenyezi Mungu.

Miongoni mwa mambo ambayo wanasayansi wamefanikiwa ni kuweza kuandaa mazingira ambayo wanadamu wanaweza kupunguza athari zinazoweza kutokea ni kuchukua tahadhari za aina mbali mbali wanapobaini ishara za maafa mapema. Kwa mfano; utabiri wa hali ya hewa umeweza kwa kiasi kikubwa kunusuru maisha ya watu wengi kwa kuchukua hatua zinazofaa pale wanapoarifiwa uwezekano wa kutokea machafuko ya hali ya hewa wanapokuweko safarini.

Watengenezaji wa vyombo vya baharini na angani wameweza kuweka mavazi ya kujiokolea pale kwa bahati mbaya inapotokezea dharura ya kufanya hivyo. Kwa ustadi mkubwa taarifa pamoja na mafunzo maalum hutolewa kwa abiria wanaosafiri jinsi ya kuyatumia mavazi hayo yaliyowekwa kwenye sehemu mbali mbali ndani ya chombo wanachosafiria.

Historia inaonesha kuwa katika mataifa yaliyoendelea kimbunga na mafuriko vinaoneka kuongoza katika maafa ya kimaumbile. Hali hii inasababishwa na sehemu ya nchi husika kijiografia pamoja na mabadiliko ya tabia nchi. Lakini maafa makubwa katika nchi nyingi zinazoendelea yameonekana kusababishwa na binaadamu wenyewe kutokana na kuharibu mazingira ikiwemo ujenzi holela hasa katika miji mikuu.

Mafuriko katika mji wa Zanzibar na maeneo jirani limekuwa jambo la kawaida kila mvua kubwa zinaponyesha. Msingi wa tatizo hilo ni ujenzi holela usiozingatia mipango miji. Matokeo ya ujenzi huo ni kuziba kwa njia zinazopitisha maji, vyoo kujaa



maji na hatimaye kuenea kwa maradhi ya miripuko. Ni dhahiri katika hali hiyo jamii hupoteza umakini wa kufanya shughuli zake na mchango wa wananchi katika maendeleo ya taifa hupungua kwa kiasi kikubwa.

Katika kukabiliana na hali hiyo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikichukua juhudi maalum kuwasisitiza wananchi kuepuka kujenga kwenye maeneo yenye kutuama maji, kwenye njia za maji na kwa kadri inavyowezekana kufuata ushauri unaotolewa na wataalamu wa mipango miji.

Hata hivyo, ongezeko la idadi ya watu mijini linaonekana wazi kutokwenda sambamba na kasi ya mahitaji ya makaazi bora ya wananchi, jambo ambalo linapelekea watu kujenga bila ya kufuata ushauri unaotolewa na wataalamu.

Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mama Mwanamwema Shein hivi karibuni alifanya ziara ya kwenda kuwapa pole waathirika wa maafa ya mvua kubwa iliyonyesha usiku wa Jumamosi kuamkia Jumapili ya Aprili 16, 2016 huko Mwanakwerekwe `C` Wilaya ya Magharibi `B`.

Katika mazungumzo yake na waathirika wa maafa hayo, alisema majanga ya kimaumbile kama vile ya mvua huweza kutokea wakati wowote ambapo mwananadamu anakuwa hana maandalizi nayo. Katika hali hiyo jamii inapaswa kushikamana kuchukua hatua za dharura kuwasaidia waliopatwa na maafa hayo licha ya wajibu wa Serikali unaotekelezwa kupitia taasisi zake mbali mbali ikiwemo Idara inayoshughulikia maafa.



***Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar Ali Juma Hamad akitoa maelezo ya maendeleo ya kambi ya waliothirika na mafuriko wakati alipofika kuwatembelea na kuwafariji katika Skuli ya Mwanakwerekwe C Wilaya ya Magharibi B Unguja, tarehe 03 Mei, 2016***

"Majanga ya aina hii yanatokana na kudura za Mwenyezi Mungu, hivyo jamii inapaswa kushirikiana bega kwa bega katika kuwasaidia wale wote watakaopata majanga ya aina hiyo kwani athari ya maafa haya inaweza kumfika kila mmoja wetu" alisema mama Mwanamwema.

Mke huyo wa Rais wa Zanzibar aliipongeza Kampuni ya Teknoljia ya Mawasiliano ya ZTE kwa msaada wao walioutoa kwa ajili ya waathirika wa maafa hayo, ambayo kwa njia moja au nyengine itaweza kuwasaidia kuwarejesha katika mwenendo wa wa maisha yao ya kawaida.

Misaada iliyotolewa na Kampuni hiyo kutoka China ni pamoja na vifaa vya kufanyia usafi, vyakula, vifaa vya masomo zikiwemo sare za skuli, kanga na mashuka ambavyo kwa jumla vina thamani ya shilingi milioni 42.9. Msaada huo mkubwa umetolewa kupitia Umoja wa wake wa Viongozi. Zaidi ya msaada huo, misaada mingine mingi ilitolewa na taasisi mbali mbali, mashirika binafsi, vyama vya siasa na watu binafsi, hali ambayo iliondoa usumbufu kwa waathirika kwenye kambi hiyo ya Skuli ya Mwanakwerekwe C.

Maafa yaliyotokana na mvua hizo za masika kwa mara nyengine yanatoa fursa kwa jamii kujifunza athari za kujenga mabondeni. Lakini zipo taarifa za uhakika kwamba baadhi ya familia zilizoathirika na kuhamishiwa kwenye kambi hiyo ya skuli ya Mwanakwerekwe C, zimetamani kuendelea kuishi kwenye kambi hiyo kutokana na huduma nzuri zilizokuwa zikitolewa na Serikali katika kipindi chote ambacho waathirika walikuwepo kambini ikilinganishwa na huduma wanazozipata kwenye makazi yao ya asili.

Hata hivyo, siyo sahihi kuzifanya huduma bora zitolewazwo kwenye kambi za maafa kuwa kichocheo cha kuendelea kujenga na kuishi kwenye maeneo hatarishi, kwani uzoefu unaonesha kuwa maafa ya aina hiyo yanakuja na maradhi mabaya ya miripuko yanayopelekea vifo vya watu wengi.

# Matukio mbali mbali katika Picha



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimkabidhi zawadi ya fedha taslim shilingi laki tano Nd. Yunus Sose Hassan kutoka Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akiwa mfanyakazi bora Chama cha ZUPHE katika sherehe za Siku ya wafanyakazi Duniani zilizofanyika katika ukumbi wa Salama Bwawani Mjini Unguja, tarehe 01 Mei, 2016*



*Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akiwa katika picha ya pamoja na Ujumbe wa Maofisa wa Kampuni ya ZTE na baadhi ya wajumbe wa Umoja wa wake wa Viongozi mara baada ya kupokea misaada ya vitu mbali mbali kwa ajili ya wananchi walioathiriwa na mafuriko. Hafla hiyo ilifanyika Ikulu ndogo ya Migombani, tarehe 03 Mei, 2016*




*Wazazi, Walimu na Wanafunzi wa Vyuo mbali mbali waliohudhuria Ufunguzi wa Mashindano ya Tamasha la Michezo ya Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu Zanzibar yaliyofanyika katika Uwanja wa Amaan Mjini Unguja ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, tarehe 21 Mei, 2016*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambae pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo ya ushuhuda kutoka kwa Sheha wa Shehia ya Maziwa Ngo'mbe Wilaya ya Micheweni Pemba Bi. Asha Yussuf Hassan (katikati) aliyevunjiwa nyumba yake na watu wasiojulikana hivi karibuni kwa sababu za kisiasa pamoja na kukatiwa Migomba yeke wakati alipomtembelea kuangalia maafa hayo tarehe 31 Mei, 2016*

*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Ujumbe wa Chama cha Kikoministi cha China kutoka Kamati ya Jimbo la Jiangsu ukiongozwa na Katibu wake Bw.Luo Zhijon, ulipofika Ikulu Mjini Zanzibar, tarehe 02 Juni, 2016*





*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiteta jambo na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan wakati wa hafla ya kukabidhi Ripoti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania(NEC) katika ukumbi wa Mikutano Ikulu ya Dar es Salaam, tarehe 23 Juni, 2016*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Sein akizungumza na Balozi Mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China anayefanyia kazi Zanzibar Mhe. Xie Yunliang alipofika Ikulu Mjini Zanzinar kwa ajili ya kumuaga baada ya kumaliza mda wake, tarehe 14 Juni, 2016*

# Balozi Xie Yunliang amemaliza muda wake

Balozi Mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China anayefanyia kazi Zanzibar Mheshimiwa Xie Yunliang amemaliza muda wake wa kazi na anarejea nyumbani China akiwa ameacha majonzi makubwa miongoni mwa wananchi wa Zanzibar, hasa Umoja wa Wake wa Viongozi wa Zanzibar kutokana na ushirikiano mkubwa aliouonesha yeye na Mke wake wakati wote alipokuweko hapa Zanzibar.

Mheshimiwa Xie Yunliang na Mkewe Bibi Wu Yan wataendelea kukumbukwa kutokana na ukaribu wao na misaada mbali mbali ambayo siyo tu ilidhihirisha udugu wa kihistoria kati ya Zanzibar na Jamhuri ya Watu wa China, lakini ulienda mbali zaidi kwa kuonekana kubeba hisia za kibinadamu kwa kutoa misaada kwa makundi ya watu wenye mahitaji maalum wakiwemo wanawake.

Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein ambaye anaongoza Jumuiya ya Wake wa Viongozi, alionekana katika nyakati tofauti akishirikiana na Mke wa Balozi huyo Bibi Wu Yan katika kuvisaidia vikundi vya wanawake wajasiriamali, hatua ambayo imewezesha wanawake wengi kuimarisha vikundi vyao vya uzalishaji mali hasa wale wa vijijini Unguja na Pemba.

Bibi Wu anaondoka kurejea nchini China, lakini ataendelea kukumbukwa Zanzibar kutokana na kujijengea historia nzuri iliyotokana na jitihada zake zilizomfanya kusafiri hadi Kisiwani Pemba akifuatana na Mama Mwanamwema Shein, Mama Asha Suleiman Iddi na viongozi wengine wakiwemo wabunge na wawakilishi wa CCM.

Katika ziara zake vijijini Unguja na Pemba, Bibi Wu Yan alipata fursa ya kujumuika na wananchi wa Zanzibar hasa wanawake na kushuhudia hafla mbali mbali za makabidhiano ya vifaa vya aina tofauti vikiwemo vya kilimo, mifugo, upandaji wa miti, vifaa vya michezo na fedha taslim.

Katika nyakati tofauti Bibi Wu Yan alipongeza juhudi zinazochukuliwa na uongozi wa Jumuiya ya Wake wa Viongozi kwa jitihada za kikundi hicho katika kuwapatia maendeleo wanawake wa Zanzibar hasa vijijini.



*Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akizungumza na Mke wa Balozi Mdogo wa China Bibi Wu Yan katika Ikulu ndogo ya Migombani Zanzibar, tarehe 3 Mei, 2016*

# Jitihada za Serikali katika kukabiliana na tatizo la ajira.



***Wajasiriamali mbali mbali wakionesha bidhaa walizozitengeneza kwenye kituo cha kulelea wajasiriamali kilichopo Mbweni nje kidogo ya mji wa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya mafunzo yao waliopatiwa kwenye kituo hicho***

Ajira ni suala ambalo limekuwa agenda kuu nchini Tanzania na duniani kote kutokana na athari kubwa ya kiuchumi na kijamii inayopatikana kutokana na watu wengi kukosa sehemu za kufanya kazi halali. Kutokana na umuhimu wake, suala la ajira limekuwa moja kati ya mada zenye kujadiliwa sana kwenye semina, kongamano na mikutano ya kitaifa na kimataifa.

Kwa mujibu wa Shirika la kazi duniani (ILO), mtikisiko wa uchumi uliyoikumba dunia kwenye miaka ya 2000, kwa kiasi kikubwa umechangia kuongezeka kwa tatizo la ajira ambapo watu waliokosa kazi duniani waliongezeka kutoka watu milioni 178 mwaka 2007 hadi kufikia watu milioni 212 mwaka 2009. Kulingana na taarifa ya shirika hilo inayopatikana kwenye mitandao, Mataifa yaliyoathirika zaidi na hali hiyo ni yale yaliyokumbwa na mtikisiko mkubwa wa kiuchumi kama vile Ugiriki, Hispania na Italia.

Takwimu za ILO zinaonesha kuwa hali mbaya ya ukosefu wa ajira iliikumba Ugiriki ambako kwa mujibu wa takwimu za Shirika hilo la kazi Ulimwenguni, mwaka 2008 ukosefu wa ajira ulikuwa asilimia 7.7 lakini uliongezeka kuwa mbaya kila mwaka hadi kufikia asilimia 17.7 mwaka 2011.

Hali kama hiyo ililikumba taifa la Hispania ambako mwaka 2007 kulikuwa na ukosefu wa ajira asilimia 8.2 na kuongezeka hadi kufikia asilimia 26.1 mwaka 2013. Aidha, nchini Italia tatizo la ajira liliongezeka kutoka asilimia 6.1 mwaka 2007 hadi kufikia asilimia 12.2 mwaka 2013.

Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina hali mbaya sana katika tatizo hilo ikilinganishwa na baadhi ya nchi nyingi nyengine za Bara la Afrika na kwengineko duniani. Kwa mujibu wa Mkuza II (Successor Strategy of Mkuza II, Feb 2016), tatizo la ajira kwa vijana Zanzibar ni 14.3% tu, wakati nchini Afrika ya Kusini ni asilimia 26.7 (2016), nchini Mali ni asilimia 30.0 (2013), Sudan asilimia 13.6 (2014), Uturuki asilimia 11.1 (2016).

Pamoja na tatizo hilo kuonekana kuwa dogo ikilinganishwa na nchi nyengine duniani, Serikali imekuwa ikichukua juhudi mbali mbali za kukabiliana na tatizo la ajira, ambapo sekta ya viwanda ndiyo iliyoonekana kuwa na uwezo mkubwa wa kuwakomboa wananchi kuondokana na tatizo hilo.

Imeelezwa kwenye Ilani ya CCM kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kwamba, ili kuendeleza shughuli za

viwanda na biashara na kuinua uchumi wa Zanzibar, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, serikali itachukua hatua mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuandaa mkakati wa kuendeleza sekta binafsi pamoja na program ya kuwakuza wawekezaji wa ndani na wajasiriamali wadogo na wakati (SMEs ) kwa kuwapatia mafunzo, mitaji na huduma za kiufundi ili kuzalisha bidhaa bora zenye kuweza kukabili ushindani wa soko la ndani na nje ya nchi.

Aidha, serikali imepanga kuendeleza viwanda katika maeneo huru ya uchumi, maeneo maalum ya kiuchumi (SEZ) na kuwavutia wawekezaji wenye mitaji mikubwa kuwekeza miundombinu ya viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi vikiwemo viwanda vya kushona nguo, usindikaji mazao, usindikaji samaki na viwanda vya kusarifu mazao ya kilimo na mifugo.

Vile vile, Serikali imepanga kufanya mapitio ya sera ya biashara ya mwaka 2006, kuandaa sera mpya ya biashara na kuanzisha chombo maalum cha kuwaendeleza wajasiriamali wadogo na kufanya utafiti juu ya gharama za biashara kwa lengo la kuchochea ukuaji wa biashara na kuondosha urasimu katika utoaji wa leseni.

Uanzishwaji wa kituo cha kulelea na kukuza wajasiriamali Mbweni ni moja tu kati ya mipango ya serikali ya kujaribu kupunguza au kuondosha kabisa tatizo la ajira Zanzibar. Kituo hiki kilianzishwa mwaka 2015 lengo kuu likiwa ni kuwapa ujuzi vijana na wanawake kuhusu namna bora ya kukabiliana na matatizo ya ajira, kuendeleza mawazo yao ya biashara na kuyakinisha ndoto zao za kuwa na biashara endelevu.

Vituo vingine vilivyoanzishwa na Serikali kwa madhumuni yanayofanana na hayo ni kituo cha Mafunzo ya Amali kilichopo Mkokotoni katika Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na kituo cha Elimu Mbadala kilichopo Rahaleo Mjini/Magharibi Unguja na kituo cha Mafunzo ya Amali Mwanakwerekwe, Wilaya ya Magharibi B. Vile vile kituo kingine kiko Vitongoji, Mkoa wa Kusini Pemba. Serikali ina mpango wa kuanzisha kituo chengine cha kulelea na kukuza wajasiriamali (incubator) kwa



*Mwalimu Yahya Watuta kutoka Chuo cha Kilimo Mzumbe akiwaelekeza wajasiriamali namna ya kutengeneza bidhaa zitokanazo na maziwa kama vile Samli, Mtindi na nyenginezo*

upande wa Pemba ambacho kitakuwa maalum kwa ajili ya usarifu wa mazao ya kilimo (Agribusiness Incubator) ili kuongeza thamani ya mazao kwa wakulima na kupunguza tatizo kubwa la kuharibika kwa mazao. Aidha, tayari Serikali imeshatiliana saini mkataba na wakandarasi hivi karibuni kwa ajili ya kujenga vituo vipya vya mafunzo ya amali huko Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja na Daya-Mtambwe Mkoa wa Kaskazini Pemba ili kuwafunza vijana ujuzi wa kazi mbali mbali za amali.

Pamoja na mambo mengine, malengo makuu ya kituo cha kulelea wajasiriamali cha Mbweni, ni kupunguza tatizo kubwa la ajira kwa Vijana hasa baada ya kuzingatia ukweli kwamba sekta rasmi pekee haitoweza kuchukua vijana wote ambao wana uwezo wa kufanya kazi. Hivyo, sekta isiyo rasmi ina jukumu la kuzalisha wajasiriamali ambao watakuwa na uwezo wa kuanzisha biashara na kuweza kuajiri vijana wengine katika kuzalisha bidhaa na huduma mbali mbali.

Kwa kuwa kituo hiki kinatoa taaluma ya ujasiriamali, kitasaidia kupunguza tatizo la kuanguka kwa biashara (business Failure) kwani utafiti umeonesha kuwa biashara nyingi za wajasirimali wadogo na wakati huwa zinafungwa katika mwaka wao wa mwanzo kutokana na ukosefu wa elimu juu ya uendeshaji wa biashara, kutokuwa na mpango wa biashara, kutokuwa na elimu juu ya uongozi wa biashara na elimu ya utunzaji wa kumbukumbu na ukadiriaji wa bei za bidhaa zao.

Kituo hiki kina jukumu la kuwatayarisha vijana kwa kuwapa mbinu na elimu mbali mbali ambazo zitawafanya wakabiliane vyema na changamoto za biashara hususan katika miaka miwili ya mwanzo ya kuanza biashara kwani katika kipindi hiki biashara nyingi zinakufa.

Kutumia mbinu maalum za kuwabadilisha vijana kisaikolojia ili hatimaye wenyewe kwa hiari yao waweze kuona kuwa ujasiriamali ni fursa ya maisha yao. Jukumu hili limeonekana kuwa linahitaji msukumo maalum kutokana na vijana wengi kuona kuwa ujasiriamali ni kazi ya mwisho inayofanywa na wajasiriamali baada ya kutofanikiwa juhudi zao zote za kutafuta ajira kwenye sekta rasmi. Jamii imejenga dhana kwamba ujasiriamali ni kazi inayofanywa kwa sababu tu hakuna njia nyengine ya mtu kumtoa katika umasikini.

Bila ya shaka, dhana hiyo iliyojengeka katika jamii haileti tija katika kukuza uchumi wa nchi kwani katika kila ajira 10 basi nafasi 9 kati ya hizo zinatokana na sekta ya ujasiriamali. Hivyo vijana wanatakiwa kuwezeshwa kuzitambua fursa zilizomo katika ujasiriamali na kuweza kuzitumia. Kwa msingi huo kituo kina jukumu la kubadilisha ufahamu wa vijana kuwatoa walipo kama watafuta




***Matunda na mazao ya aina tofauti yanayotumiwa na wajasiriamali wanaojifunza kwenye kituo cha kulelea wajasiriamali kutengenezea bidhaa mbali mbali kama zinavyonekana baadhi yake ziko tayari kwa matumizi ya binaadamu***

kazi na kubadilika kuwa wazalisha kazi.

Kituo hiki kimedhamiria kuunganisha sekta zinazotoa nafasi kubwa za ajira na vijana hasa baada ya kutambua kuwa vijana wengi wa sasa hawapendi kilimo, sekta ambayo ndiyo yenye kutoa nafasi kubwa ya ajira. Hivyo kituo cha kulelea wajasiriamali kina jukumu la kuwaunganisha vijana na sekta hizi kwa kuwapatia mafunzo ya kusarifu mazao ya kilimo ambayo faida yake hupatikana haraka haraka tofauti na kilimo chenyewe. Hali hii inachangia kuhamasisha sekta za uchumi katika nchi na kupelekea maendeleo endelevu.

Kituo kina jukumu la kutayarisha vijana ambao wataweza kuanzisha viwanda vidogo na vya kati kama muelekeo wa uchumi wa Zanzibar kwenda katika uchumi wa kati. Ili kufikia lengo hilo, vijana wanatakiwa waone fursa zilizopo katika viwanda vidogo na wajue jinsi ya kuanzisha na kusimamia viwanda hivyo.

Katika kituo cha kulea na kukuzia wajasiriamali, kuna mashine mbali mbali zenye kufanyakazi tofauti. Miongoni mwa mashine hizo ni mashine za kusagia nafaka ambazo katika kituo hicho zinatumika kujifunza namna ya kusaga na kuchanganya aina tofauti za viungo "Spices" na kujua harufu inayopatikana baada ya mchanganyo wa aina tofauti za viungo.

Mafunzo haya ya uchakataji wa viungo yanawawezesha wajasiriamali kuongeza thamani ya viungo vilivyozoeleka kwa kupata harufu mpya ambayo, iwapo ikitokea kupendwa na watumiaji wengi, basi fomula iliyotumika kuchanganya viungo hivyo inabaki kuwa mali ya mjasiriamali aliyeitengeneza.

Kuna mashine ya kusarifu asali ambayo inatumika kuchemshia asali na kuchuja asali ambapo mabaki yanayotokana na asali hutumika kutengenezea bidhaa nyengine kama vile mishumaa. Asali safi huhifadhiwa katika kifungashio mfano chupa kwa ajili ya kuuzwa. Wajasiriamali wanafundishwa pia namna ya kutumia malighafi nyengine inayotokana na asali kama vile nta, ambayo hutengenezewa mishumaa. Wajasiriamali hutengeneza mishumaa ya aina na harufu tofauti kutegemea na vifaa pamoja na malighafi wanayotumia.

Ipo mishumaa yenye harufu ambayo inapochomwa hutoa harufu ya udi na viungo vingine vinavyopatikana Zanzibar mfano mchaichai, karafuu na mkaratusi. Vile vile ipo mishumaa ya dawa ya mbu (mosquito Repellent) ambayo moshi wake unatumika kufukuzia mbu. Kuna soko la kutosha la kuuzia mishumaa hii. Wajasiriamali wamegundua soko la uhakika kwenye hoteli za kitalii.

Kwenye kituo hiki kuna mashine za kusarifu maziwa, ambazo hutengeneza mtindi, samli na "cheese". Kabla ya wajasiriamali kutumia mashine hizi, hupatiwa mafunzo maalum ya kusarifu maziwa, ambapo kwa mujibu wa wanafunzi hao, utaratibu uliozoeleka wa kuuza maziwa bila ya kufanyiwa usarifu hauwasaidii sana wafugaji kwani faida inayopatikana ni ndogo sana na hivyo hawana budi kubadilika ili waweze kupata faida kubwa zaidi.

Zipo pia mashine za kutengenezea sharbati (juisi). Mashine hizi zinatengeneza aina zote za sharbati za matunda kama vile machungwa, embe, ndimu, pensheni na aina nyengine zote kutegemea na mahitaji ya mjasiriamali.

Wajasiriamali pia hufundishwa namna ya kutengeneza "jam na tomato source". Taaluma hii kwa wajasiriamali ni mkombozi wa mazao mengi yanayopatikana kwa wingi Zanzibar. Uzoefu umeonesha kuwa wakati wa msimu mkubwa wa baadhi ya mazao, mazao mengi huharibika kutokana na kukosa watumiaji na pia kukosa sehemu za kuyahifadhi au mbinu mbadala za kuyatumia.

Kuna mashine ya kukaushia ambayo inatumiwa kukaushia matunda, dagaa, mboga za majani na aina nyengine nyingi za bidhaa bila ya kupoteza uasilia wake.

Moja kati ya matatizo makubwa ya muda mrefu ya wajasiriamali wa Zanzibar ni kukosa ujuzi, maarifa na ustadi wa kufunga bidhaa zao wanazozitengeneza na kuweza kuuzika kwenye masoko. Hali hiyo inasababisha bidhaa nzuri kushindwa kuuzika kutokana na ushindani uliopo kuanzia hatua ya utengenezaji bidhaa hadi kuziuza.

Akizungumzia kuhusu mipango ya baadae ya kituo hicho, Mkurugenzi uendeshaji wa kituo hicho Bwana Said amesema wanakusudia kunazisha kituo cha kulea na kukuza wajasiria mali ( incubator)Pemba, kuanzisha kituo cha Incubation kwa ajili ya kufanya "Recycle ya Plastic, paper na Glass" pamoja na utengenezaji wa makaa na vifaa vinavyotokana na taka(Green Technology Incubator).

Aidha, amesema wanakusudia kuanzisha programu ya kusaidia "Incubator" kujitegemea na kuwasaidia wajasirimali baada ya kumaliza mafunzo yao (Expansion of Incubator and establishment of Accelerator Programme).

# Mtazamo wa Wananchi kwenye bajeti ya Serikali 2016/17

Mwezi Mei mwaka huu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewasilisha katika Baraza la Wawakilishi mwelekeo wa hali ya uchumi 2016 na mpango wa maendeleo 2016/17 pamoja na mapendekezo ya bajeti kuhusu mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, Serikali ilielezea mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka uliopita 2015/16 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka 2016/17.

Kuwasilishwa kwa bajeti hiyo kumefanyika chini ya miezi miwili baada ya wananachi wa Zanzibar kufanya tukio la kihistoria la kisiasa, kutokana uamuzi wao wa kumchagua tena Dk. Ali Mohamed Shein kuwa Rais wa Zanzibar kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Maamuzi hayo ya Wazanzibari yalifanywa kwenye uchaguzi mkuu wa marudio uliofanyika Machi 20,2016.

Uamuzi wa kumrejesha tena madarakani Dk. Ali Mohamed Shein kwa njia ya kura, siyo tu ulitokana na wananchi kuridhishwa na uongozi wake katika kipindi cha kwanza cha miaka mitano iliyopita, lakini vile vile ulitokana na Ilani ya chama chake ya mwaka 2015 – 2020, ambayo yeye na wenzake kupitia chama chake, waliinadi wakati walipokwenda kwa wananchi hao kuomba ridhaa ya uongozi kwa kipindi hicho.

Kwa mujibu wa hali ya mwelekeo wa uchumi 2016 na mpango wa maendeleo 2016/17, mwelekeo wa uchumi unatarajiwa kwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya maendeleo ya 2020, Mkakati mpya wa maendeleo 2016 - 2020, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 na hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, ambayo aliitoa katika uzinduzi wa Baraza la tisa la Wawakilishi. Ni dhahiri wananchi wengi walikuwa wakisubiri kwa hamu kuona hatua za kwanza za Serikali katika kutekeleza yale ambayo waliahidiwa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu uliopita.

Hivyo, Bajeti ya Serikali ambayo inakwenda sambamba na mwelekeo wa hali ya uchumi 2016 na mpango wa maendeleo wa 2016/17 kwa vyoyote vile imegusa hisia na matarajio ya wananchi wengi wa Zanzibar.

Ukweli ulio wazi kwamba katika awamu ya kwanza ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein, Zanzibar ilipata mafanikio makubwa ya kupigiwa mfano katika sekta zote na hasa ukuaji wa uchumi. Katika kipindi hicho takwimu zinaonesha kuwa uchumi wa Zanzibar ulikuwa kwa wastani wa asilimia 7.0. Hali hiyo ilichangiwa na mambo mengi ikiwemo utulivu wa kisiasa, amani na mshikamano wa wananchi.

Lakini matarajio makubwa ya wananchi wa Zanzibar kutokana na bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017, yamejiegemeza zaidi kwenye mustakabali wa uchumi na mapato hasa kwenye mwelekeo wa Serikali kiuchumi, wakiamini kuwa kukua kwa uchumi ndiko pekee kutakakowatoa katika tatizo la umasikini.

Akizindua Baraza la tisa la Wawakilishi la Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alielezea haja ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi ili isipungue asilimia nane (8%) kwa mwaka, ambapo jitihada zielekezwe katika kushajiisha uwekezaji, uimarishaji wa sekta za uchumi kama vile huduma husuan utalii, mageuzi ya viwanda na kilimo, ikiwemo cha mazao, ufugaji na uvuvi.

Ni dhahiri mageuzi hayo ya kiuchumi yataletwa kupitia utekelezaji wa mkakati mpya wa maendeleo uliochukua nafasi ya MKUZA II, ambao moja ya eneo muhimu la matokeo ya mkakati huu mpya ni la mageuzi ya kiuchumi.



Inatia moyo kuona kuwa mustakabali wa mapato ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano ijayo, umejikita zaidi katika kuimarisha uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani. Mwelekeo huo unaendana na dhamira ya Serikali ya kuongeza uwezo wa kujitegemea na kwa kadiri inavyowezekana kupunguza utegemezi wa washirika wa maendeleo kuhudumia bajeti ya Serikali. Hii ni dhamira ambayo ilianza kuoneshwa na Dk. Ali Mohamed Shein wakati wa kipindi cha kwanza cha miaka mitano ya uongozi wake.

Dk. Shein, mara kadhaa katika kipindi chake cha kwanza cha uongozi, alikaririwa akiwaambia wananchi kuacha kutegemea wafadhiili kwa kila kitu hata kwa ile miradi ambayo iko ndani ya uwezo wao. Katika kuhakikisha kuwa suala hilo linawezekana, aliongoza harambee katika vijiji mbali mbali ambapo fedha nyingi zilizopatikana zilisaidia kukamilisha miradi ya ujenzi wa skuli, hospitali na hata masoko ya kuuzia bidhaa za wananchi.



*Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakiwa wamesimama katika moja ya shughuli zao za kila siku zinazoendelea katika Baraza hilo liliopo Chukwani Wilaya ya Magharibi B Unguja*

Suala kubwa ambalo linaonekana kuleta changamoto katika ukuaji wa uchumi wa Zanzibar, ni mtikisiko wa uchumi katika mataifa yaliyoendelea ambayo uzoefu umeonesha kuwa athari za nchi hizo huingia na kusambaa kwenye mataifa yanayoendelea.

Kwa mujibu wa mwelekeo wa uchumi, ukuaji wa uchumi Zanzibar katika mwaka huu wa fedha unatarajiwa kufikia asilimia 6.3 ambayo ni chini ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo uchumi ulikua kwa asilimia 6.6.

Kutokana na hali hiyo, indhari inatolewa kwamba jamii inapaswa kujipanga ili iweze kukabiliana na changamoto zenye kupelekea kupungua kasi ya ukuaji wa uchumi hasa kwa yale mambo ambayo yamo ndani ya uwezo wa wananchi. Miongoni mwa changamoto ambazo zinatarajiwa kuathiri kasi ya ukuaji wa uchumi, ni uwezekano wa kupungua mazao yanayotokana na kilimo.

Hivyo, jitihada za makusudi zinahitajika kwa wakulima wa Zanzibar kufuata kikamilifu ushauri wa wataalamu wa kilimo, kwani ushahidi umeonesha kuwa kilimo cha kisasa kwa kiasi kikubwa kinakuwa na tija hasa pale wakulima wanapofuata kikamilifu ushauri wa wataalamu hao pamoja na kutumia pembejeo inavyostahiki. Hivyo pamoja na tatizo hilo kuwa kubwa duniani, mabadiliko katika kilimo yanaweza kusaidia katika kukabiliana na changamoto hii.

Sababu nyengine ni kupungua kwa shughuli za usafirishaji wa bidhaa kutokana na kuwa mwaka 2016 ni msimu mdogo wa uzalishaji wa zao la karafuu. Hata hivyo, Zanzibar inayo faida ya ziada ya zao hili mwaka huu ikilinganishwa na miaka iliyopita. Wananchi hawana budi kujivunia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kuimarisha zao hilo ndani ya miaka mitano iliyopita. Katika kipindi hicho, kulikuwa na mikarafuu mingi mipya iliyopandwa ambayo baadhi yake imeshafikia umri wa kuanza kuzaa. Aidha, biashara ya magendo ambayo haina tija kwa Serikali na wananchi ilipungua kwa kiasi kikubwa.

Ni dhahiri iwapo fursa hizo zitatumika vyema, athari ya kupungua kwa shughuli za usafirishaji wa karafuu haitaonekana kuwa kubwa sana. Lakini kinyume chake hujuma za kuchoma mikarafuu kama zilivyoanza kuonekana kisiwani Pemba, zinaweza kuzidisha athari itakayotokana na changamoto hiyo. Ni vyema wananchi wote hususan raia wema wakatoa ushirikiano katika kukabiliana na vitendo vyote vya hujuma dhidi ya mikarafuu.

Changamoto nyengine kubwa inayotarajiwa kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi ni kupungua kasi ya kukua uchumi kwa nchi zenye uchumi mkubwa duniani hususan nchi zilizo katika Zoni ya Ulaya, ambazo zina mchango mkubwa katika soko la utalii la Zanzibar. Miongoni mwa nchi hizo ni Itali, Ujerumani, Hispania, Ubelgiji na Ufaransa.

Uk.18

Ili kuziba pengo hili, Kamisheni ya Utalii Zanzibari haina budi kuendelea kupanua wigo wa kutangaza zaidi utalii wa Zanzibar kwa kutilia maanani vivutio vya utalii ambavyo vinapatikana Zanzibar pekee, sambamba na kuimarisha utalii wa ndani.

Takwimu za hivi karibuni zinaonesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2015, licha ya idadi ya watalii kupungua kwenye mataifa mengi ya Bara la Afrika, na licha ya kuwa kipindi hicho ni kipindi cha uchaguzi mkuu, Zanzibar iliongoza kwa kuwa na watalii wengi hasa wale wanaofika Zanzibar moja kwa moja kutoka kwenye nchi zao. Hali hiyo inaonesha kuwa Zanzibar ni visiwa vinavyopendwa na watalii.

Katika kufanikisha suala la utalii, amani, utulivu na mshikamano yataendelea kuwa ni masuala muhimu katika nchi na kwamba Serikali ina wajibu wa kuchukua hatua zote muhimu kuhakikisha kuwa amani inadumu nchini.

Bajeti ya mwaka 2016/17 inahamasisha wafanyakazi na wananchi wote kwa jumla kufanyakazi kwa bidii zaidi, kuzidisha kubana matumizi na kufanya matumizi kwa yale mambo ambayo tija yake itakuwa inaonekana. Kadhalika, jamii hainabudi kukubali kufanya kazi kwa kujitolea ili kuhakikisha kuwa Zanzibar inapiga hatua kubwa mbele kimaendeleo, jambo ambalo linawezekana iwapo kila mtu atakuwa na dhamira ya dhati ya kutaka kujitegemea.

# ZSSF inavyoendelea kustawisha mji wa Zanzibar



***Ramani inayoonesha jengo jipya la Treni (Chawl Building) linalotarajiwa kujengwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) mara baada ya kubomolewa jengo lililopo hivi sasa katika maeneo ya Darajani Mjini Unguja***

Miaka mitatu baada ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kukamilisha miradi kadhaa mikubwa iliyozidisha haiba ya miji ya Unguja na Pemba, harakati zimeanza za kulifanyia matengenezo makubwa jumba la treni (Chawl Building) liliopo darajani mjini Unguja bila ya kuathiri ramani yake ya asili.

Kama ambavyo umebadilika muonekano kwenye maeneo ya miradi ya ujenzi wa mnara wa kumbukumbu ya Mapinduzi katika eneo la Michenzani, ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto cha Umoja – Kariakoo na kiwanja cha kufurahishia watoto cha Uhuru Pemba, mradi huu unatarajiwa kubadilisha kabisa muonekano wa eneo la Darajani, ambapo ndipo inapoonekana sura halisi ya mji wa Zanzibar kutokana na harakati nyingi za kibiashara zinazoendeshwa na wananchi wa Zanzibar na wageni kutoka nchi mbali mbali.

Jumba hili la treni lina historia kubwa katika Zanzibar. Historia inaonesha kuwa jengo hilo lilijengwa mwaka 1880 na limekuwa likitoa mchango mkubwa katika kukuza sekta



*Jengo la Treni (Chawl Building) lililopo eneo la Darajani Mjini Unguja linalosubiri kubolewa na kupisha ujenzi wa jengo jengine jipya litalofanana na hili kwa ramani yake. Jengo hilo linatarajiwa kujengwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)*

ya biashara na utalii. Lengo la kulifanyia matengenezo makubwa ni kuondoa hatari iliyopo inayotokana na uchakavu wake na uwezekano wa kuanguka na kutishia usalama wa wakazi na watumiaji wa jumba hilo.

Ripoti zilizoandaliwa na wataalamu mbali mbali wakiwemo wa Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe zinaonesha kuwa, jengo hilo la daraja la kwanza halifai kutumiwa kibiashara na makaazi ya watu kwa kipindi hichi.

Jengo hili linamilikiwa na watu watano (5) na wapangaji arobaini na mbili (42). Ghorofa ya chini kuna milango ya maduka ipatayo arobaini na saba (47) na ghorofa ya juu kuna ghala za wafanyabiashara ambazo hutumia kuhifadhia bidhaa zao. Aidha nyumba zipatazo sita (6) hutumiwa na baadhi ya wapangaji kwa shughuli zao za makaazi.

Kwa mujibu wa mipango ya ZSSF, matengenezo ya jengo hilo yanalenga kulifanya kuwa la kisasa zaidi likizingatia mahitaji muhimu ya watumiaji wake kwa wakati tulionao. Mpango wa kwanza ni kuhakikisha kuwa matumizi ya asili ya jengo hilo yanakuwepo ikiwemo maduka, nyumba za kuishi na ghala za kuhifadhia mizigo ya wapangaji.

Mpango wa pili ni kuongeza huduma nyingine ili biashara na maakazi yawe na mvuto wa kipekee. Hii inajumuisha kuongeza "mini supermarket", maduka ya kisasa ya kujitegemea, sehemu za kufanya mazoezi (gym), mkahawa wa kisasa, sehemu za ofisi, huduma za lifti tatu, mifumo ya ulinzi (CCTV), mifumo ya tahadhari za moto, mifumo ya viyoyozi n.k.

Jengo hili pia litawekwa "solar panel" zitakazosaidia mahitaji ya umeme unaotokana na nguvu za jua. Kwa eneo la nje ya jengo, ZSSF imejipanga kuweka huduma ya maegesho ya magari itayozungukwa na bustani mwanana kwa wananchi watakaopenda kupumzika nyakati za jioni. Eneo hilo pia litatumika kuhifadhi majenereta ya uhakika inapotokezea umeme kukatika.

Utekelezaji wa mradi huu ni miongoni mwa utekelezaji wa Ilani ya CCM 2015-2020 kwa ZSSF ambayo imepanga kuimarisha mfuko wa Hifadhi ya Jamii ili uendelee kuwekeza katika miradi mbali mbali ya kiuchumi inayozalisha faida kubwa na kukuza mapato ya mfuko huo.



# Pemba wamefurahishwa na mradi wa barabara ya Ole-Kengeja




Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Ole hadi Kengeja ambao umelenga kuondosha usumbufu wa usafiri kwa wananchi na usafirishaji wa mazao yanayotoka maeneo mbali mbali yanayopita barabara hiyo, umekuwa ndio mazungumzo makubwa kwenye maskani na baraza nyingi kisiwani Pemba.

Mradi huo ambao umekuwa ukizungumzwa na wananchi wa rika na jinsia zote, unaonekana kuwa mkombozi hasa kwa wananchi wanaoishi katika ukanda wa mashariki mwa kisiwa cha Pemba, kutokana na uwezekano mkubwa wa kuwatoa wananchi kutoka katika dimbwi la umasikini baada ya kukamilika kwake.

Kwa mujibu wa ramani ya ujenzi wa barabara hiyo na maoni ya wananchi mbali mbali, watakaofaidika na mradi huo ni wananchi wote wa Pemba, kwani barabara hiyo itawaunganisha wananchi wa mikoa miwili ya Pemba, Mkoa wa Kaskazini na Mkoa wa Kusini Pemba na hivyo kuwarahisishia harakati zao za maendeleo kwa safari za kwenda upande mmoja hadi mwengine. Barabara hiyo itawaunganisha wananchi wa Wilaya ya Chake chake, Mkoani, Wete na Micheweni.

Bw. Moh'd Nassor Hamad ni mkaazi wa kijiji cha Ole Kiyanga amesema uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuijenga barabara hiyo ni wa kupongezwa kwani kumalizika kwake kutaweza kuwasaidia wananchi wengi kisiwani Pemba kutokana na mpangilio wa maeneo yaliyopita barabara hiyo ambao haukulenga kuwanufaisha wananchi wa eneo moja.

"Mimi binafsi naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuona umuhimu wa kuijenga barabara hiyo ambayo kwa muda mrefu ilikuwa ikiwaletea usumbufu mkubwa wananchi wa Ole na vijiji vyengine jirani" alisema Bw Hamad.

Hata hivyo Bw. Hamad ameiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuangalia kwa umakini zaidi suala la utoaji wa fidia kwa wananchi watakaoathiriwa mali zao kutokana na mradi huo kwani amesema mara nyengine fidia hizo zinakuwa hazilingani na thamani ya mali za waathirika,

jambo ambalo hatimaye husababisha wananchi kutokuwa na imani na baadhi ya watendaji.

Saidi Mbarouk Ali mfanyabiashara wa shehia ya Pujini ameelezea kufurahishwa kwake na ujenzi wa barabara ya Ole hadi Kengeja kwani amesema kuwepo kwa barabara hiyo kutaweza kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zao kutoka Pujini na vijiji nyengine kwenda mijini na kwenye masoko mengine.

"Ukweli kuwepo kwa barabara hiyo kutaweza kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zetu na shughuli zetu nyengine na hivyo kuwa kichocheo cha maendeleo, kujiongezea kipato na kupambana na umasikini", alisema Mzee Said.

Uamuzi wa kujenga barabara katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba unatokana na ukweli kwamba kuimarika wa miundo mbinu ya barabara ndio kuimarika kwa maendeleo ya kiuchumi. Hivyo, kuimarika kwa barabara hiyo siyo tu kutaweza kuimarisha maendeleo ya kiuchumi lakini vile vile kuimarisha uchumi wa Zanzibar na bila ya shaka maisha ya mtu mmoja mmoja.

Akizungumzia juu ya maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo Mkandarasi wa ujenzi wa ujenzi wa barabara ya Ole hadi Kengeja, Bwana Amini Kh. Abdullah kutoka Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (UUB) alisema barabara hiyo ni miongoni mwa barabara zilizolengwa kujengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na umuhimu wake mkubwa kiuchumi na kijamii.

Alisema barabara hiyo ina urefu wa km 35 na ameielezea kuwa Serikali iliamua kujenga barabara hiyo kutokana na kuwa ndiyo barabara pekee inayounganisha miji ya Chake chake, Mkoani pamoja na vijiji kadhaa vya Mikoa ya Kusini na Kaskazini Pemba.

Mhandisi huyo alisema kuwa barabara hiyo inajengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na mkopo wenye riba nafuu kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Nchi zinazotoa Mafuta kwa wingi (Opec Fund) na unatarajiwa kugharimu jumla ya fedha za Kimarekani Dola milioni 12, ambapo Dola milioni moja ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya ulipaji wa fidia.

Kama ilivyo miradi mingine mingi, mradi huu nao umekabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zimejitokeza wakati wa kuanza utekelezaji wake. Miongoni mwa changamoto hizo ni ucheleweshwaji wa fedha kutoka (OFID) kwa ajili ya kulipia fidia. Changamoto hiyo imepelekea kusita kidogo kwa ujenzi huo kwani Serikali imeweka utaratibu wa kutovunja nyumba za watu kwenye maeneo yanayopita barabara iwapo wakaazi wa maeneo husika hawajalipwa fidia.

Changamoto nyengine zilizojitokeza ni kuondoshwa kwa nguzo za umeme, mabomba ya maji katika baadhi ya maeneo yaliyopita ujenzi huo pamoja na uchache wa baadhi ya vifaa vya kujengea na kujitokeza kwa hali ya mvua wakati wa utekelezaji wa mradi.

Miongoni mwa vijiji ambavyo vitafaidika kwa karibu zaidi na ujenzi wa barabara hiyo ya Ole hadi Kengeja ni Uwandani, Vitongoji, Pujini, Chambani, Ukutini, Kendwa na Kengeja. Katika kipindi hiki mradi umeshalipa nyumba 9, maduka 3, vibanda 6 kazi ambayo itakuwa inaendelea ambapo inakadiriwa kiasi cha nyumba 52 zitaathirika moja kwa moja.

Mhandisi huyo ametoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Kusini hasa wale ambao maeneo yao yatapita barabara hiyo kutoa kila aina ya ushirikiano ili kuona malengo yaliyowekwa ya mradi wa ujenzi wa barabara hiyo yanakwenda vizuri na kuiepusha Serikali na vikwazo ambavyo vinaweza kuzorotesha ujenzi wa barabara hiyo.



*Sehemu ya Barabara mpya ya Ole - Kengeja inayoendelea kujengwa Kisiwani Pemba*



*Meneja wa Mradi wa Barabara ya Ole - Kengeja Amini Khalid Abdullah akielezea maendeleo ya ujenzi wa Barabara hiyo Ofisini kwake Chake - Chake Pemba, tarehe 29 Mei, 2016*

# Mabadiliko kuelekea utumishi wa umma uliotukuka yameanza rasmi

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wananchi wote wa Zanzibar kwa jumla, wamefaulu vyema mtihani mgumu wa kisiasa uliokuwa ukiwakabili kwa kipindi cha takriban miezi saba kuanzia mwezi wa Septemba, 2015 wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu hadi kumalizika kwa uchaguzi wa marudio wa tarehe 20 Machi, 2016.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein aliapishwa rasmi tarehe 24 Machi, 2016, baada ya kuchaguliwa tena na wananchi wa Zanzibar kuiongoza Zanzibar.

"Uchaguzi umekwisha na hakuna mwengine hadi mwaka 2020". Hii ni kauli ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ambayo aliitoa wakati alipokuwa akizindua Baraza la tisa la Wawakilishi tarehe 5 Aprili 2016. Sambamba na kauli hiyo, Dk. Shein alibainisha kazi kubwa inayoikabili Serikali anayoiongoza na wananchi kwa ujumla katika kipindi kijacho hadi kufikia mwaka 2020.

Kumekuwa na maoni mengi tofauti kufuatia kuanza kwa kipindi cha pili cha Dk. Shein na hasa kufuatia kurudia mara kadhaa kauli yake ya kuwataka Wazanzibari na hasa Watumishi wa Umma kubadilika na kuacha kufanyakazi kwa mazowea.

Itakumbukwa kwamba kauli hiyo aliitoa pia katika kipindi cha mwanzo cha uongozi wake, alipokuwa kwenye mkutano na viongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi baada ya kumaliza ziara yake ya kwanza kwenye maeneo mbali mbali ya Mkoa huo na kuona hali halisi ya kiutendaji.

Vile vile, itakumbukwa kuwa kabla ya kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar mara ya kwanza, Dk. Shein alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa takriban miaka 9. Lakini historia yake vile vile inaonesha kuwa, kabla ya kushika



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifungua semina ya siku mbili kwa Viongozi na Watendaji Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayohusu kukumbushana masuala mbali mbali ya kiuongozi na taratibu zake. Semina hiyo imefanyika katika ukumni wa Baraza la Mapinduzi Ikulu Mjini Unguja, tarehe 14 Mei, 2016*

wadhifa huo, aliutumia muda wake mwingi akiwa mfanyakazi wa kawaida ndani ya sekta ya umma hadi kufikia kushika nyadhifa za Uongozi wa ngazi ya juu ndani ya taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Dk. Shein baada ya kumaliza masomo yake hapa Zanzibar, alipata masomo ya elimu ya juu nchini Urusi kwa miaka sita kabla ya kwenda nchini Uingereza kwa miaka minne. Uzoefu, taaluma na maarifa ya Dk. Shein katika masuala mbali mbali, vinatosha kabisa kujua lipi lifanyike na kwa wakati gani ili kufikia malengo yaliyowekwa. Ni wazi kwamba yeye ni miongoni mwa marais wenye uelewa na ueledi wa kutosha katika utendaji na uongozi kwenye Sekta ya Umma.

Juhudi maalum zilizoonekana kuchukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa chini ya uongozi wa Dk. Shein katika kipindi cha miaka mitano ya kwanza, zilikuwa zinalenga kuweka sawa zana "Instruments" za kufanyia kazi kuelekea kwenye utumishi wa umma uliotukuka.

Miongoni mwa hatua muhimu zilizochukuliwa na Serikali ni kupitisha Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011, Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar Namba 1 ya mwaka 2012 na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Zanzibar Namba 4 ya mwaka 2015.

Kila sheria miongoni mwa sheria hizi imeweka masharti ya msingi yanayowalazimisha wahusika kuyafuata. Kwa mfano; sehemu ya pili ya Sheria ya Utumishi wa Umma imeweka masharti ya lazima ya misingi mikuu na maadili ya utumishi wa umma ambayo

kila mtumishi wa umma atatakiwa kuyasimamia na kuyatekeleza ipasavyo.

Misingi hiyo ni pamoja na kujielekeza katika malengo ya kazi, kujielekeza kwa mpewa huduma,



kujielekeza katika kushiriki na kujilekeza katika thamani ya fedha. Misingi mingine ni pamoja na ugawaji wa madaraka kwa wingi na wajibu katika kutumikia mamlaka ya nchi.

Chimbuko la Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma linatokana na Sheria ya Utumishi wa Umma kifungu cha 7, ambayo imetaja maadili yanayopaswa kufuatwa kwa kila mtumishi wa umma.

Maadili hayo yanamtaka kila mtumishi wa umma awe mwaminifu na mwenye uadilifu, afanye kazi kwa tahadhari na bidii, katika utekelezaji wa ajira ya Utumishi wa Umma, ampe kila mtu heshima na nidhamu na asibughudhiwe. Vile vile, atekeleze maelekezo halali na yanayokubalika yaliyotolewa na mtu aliyeidhinishwa na wakala wa muajiriwa ambaye ana maamuzi na mamlaka ya kutoa maelekezo hayo.

Kadhalika, mtumishi wa umma anatakiwa atunze usiri unaotakiwa wakati wa kufanya mahusiano rasmi ambayo mwajiriwa atafanya na waziri au mfanyakazi yeyote wa Wizara. Aweke wazi na achukue hatua muafaka za kuepusha mgongano na uajiri wake katika utumishi wa umma, asitoe taarifa za uongo au za kupotosha wakati anapotakiwa kutoa taarifa rasmi zinazohusiana na uajiri katika utumishi wa umma.

Kwa mujibu wa sheria ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Namba 1 ya mwaka 2012, Mamlaka hiyo imepewa uwezo mkubwa kiutendaji kuweza kutekeleza majukumu yake. Kifungu 13 (1) (b) na (c) cha Sheria hiyo, kinatoa mamlaka kwa taasisi hiyo kufanya uchunguzi. Aidha, katika kuhakikisha kuwa Mamlaka hiyo inakuwa na nguvu za kutosha za kukabili jinai ya rushwa na uhujumu wa uchumi, kifungu namba 19 (2) cha Sheria hiyo, kinatoa uwezo, fursa na kinga alizonazo afisa wa polisi katika kufanikisha taratibu za upelelezi wa jinai.

Miongoni mwa uwezo uliotolewa kisheria chini ya kifungu nambari 14 (1) hadi (7), 25 na 28 ni kukamata watuhumiwa, kufanya upekuzi wa mwili, wa majengo, vyombo vya usafiri, vya anga, vya ardhi na bahari, kuitisha kuzuia nyaraka, mali na vitu vinavyotuhumiwa, kuchunguza hesabu za benki za mtu yoyote, kuzuia hati za kusafiria, kupekua compyuta na njia nyengine za kielektroniki na kadhalika.

Sheria hizi ambazo pia zimeainisha adhabu kwa watakaokiuka sheria, zinatoa mwelekeo kwa watumishi wa umma kufanyakazi zao kwa uadilifu zaidi na kuleta matokeo yanayokusudiwa.

Miongoni mwa mambo kadhaa yaliyobainishwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kuwa ni muhimu kufanywa baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, ni pamoja na kuhakikisha kuwa wananchi wa Zanzibar na hasa watumishi wa umma wanalitekeleza kwa vitendo agizo lake alilolitoa mwaka 2011 mara tu baada ya kuingia madarakani la kuwataka wananchi kubadilika na kuacha kufanyakazi kwa mazowea.

Kauli hiyo inatokana na ukweli kwamba ingawa wananchi walibadilika, lakini bado kuna matatizo makubwa kwenye viwango vya utendaji na nidhamu kazini.

"Wapo baadhi ya wafanyakazi ambao hawapendi kufanyakazi, na wengine hawataki kufanyakazi. Lakini wao ndio wa mwanzo wanaotaka mishahara mikubwa, posho nzuri, safari za kila wakati na kuhudhuria kwenye semina na mkiutano kila mara". Alisema Dk. Shein wakati alipokuwa akizindua Baraza la tisa la Wawakilishi tarehe 5 Aprili 2016.

Tabia ya kutowajibika ipasavyo katika kazi haiko kwenye taasisi za umma pekee, lakini vile vile ni tabia iliyojenga ndani ya taasisi binafsi. Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Waajiri Zanzibar (ZANEMA) Bwana Salahi Salim Salahi amesema kuna mazowea yaliyojengeka miongoni mwa wafanyakazi wanaofanya wapendavyo bila ya kujali sheria na kanuni za kazi.


Jambo linaloonekana wazi kwamba baadhi ya wafanyakazi wanakwenda kazini siku wanazotaka, badala ya saa 42 za kazi kwa wiki, wao wanafanyakazi kwa muda wa saa 18-25 tu kwa wiki.

Wanaingia kazini kwa siku na saa wanazotaka huku wakiwa na dharura nyingi za kweli na za mipango, kutofanyakazi hadi wapewe chochote na urasimu mkubwa usiokuwa wa lazima.

Kwa msingi huo serikali sasa imefikia mahala ambapo italazimika kuchukua hatua kwa wale wote watakaoshindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

"Hatuwezi kuwa na wafanyakazi waliokuwa hawana nidhamu. Sasa basi, imetosha. Waliopewa dhamana ya kuziongoza Idara mbali mbali za Serikali watapaswa watekeleze wajibu wao kwa kuwasimamia wafanyakazi walio chini yao. Pindi kama hawatawawajibisha, basi watawajibishwa wao. Lengo letu liwe kutoa huduma kwa wananchi, kwani sote tunawajibika kwao". Alisisitiza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

# Jamhuri ya Korea na SMZ zilivyodhamiria kuondoa umasikini Zanzibar



***Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Sheuin akisalimiana na Balozi wa Jamhuri ya Korea nchini Tanzanzia Mhe. Song Geum-Young alipofika Ikulu Mjini Zanzibar kwa mazungumzo ya mashirikiano baina ya nchi hizo, tarehe 27 Juni, 2016***

Mafanikio ya serikali katika kukabiliana na changamoto ya umasikini Zanzibar yanaonekana wazi wazi katika sekta tofauti ikiwemo sekta za kilimo na uvuvi, ambazo wananchi wameamua kuziendesha kwa kutumia mbinu za kisasa na kuachana na utaratibu wa zamani wa kufanya shughuli hizo.

Haihitaji chombo maalum au elimu ya kiwango cha juu kuweza kufahamu mafanikio ya sekta ya Kilimo Zanzibar, ambayo inachangia asilimia 31 ya pato la taifa (GDP) na kuwawezesha wananchi walio wengi kujikimu kimaisha na kuwapatia uhakika wa chakula na lishe bora.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita sekta ya kilimo imefanikiwa kupitisha sheria na sera mbali mbali ikiwemo sera ya masoko na kuanza kutumika, sheria ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar na sheria ya Haki Miliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu na mimea.

Vile vile taarifa za mafanikio ya sekta hiyo zinaelezea hatua ya kuanzishwa mashamba darasa 1,200 ya wakulima sambamba na kuwapatia mafunzo wakulima 2,800 wa zao la mpunga na 1,500 wa zao la muhogo na mboga mboga. Jitihada hizi zinaenda pamoja na ongezeko la matrekta na pembejeo nyengine za kilimo katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.

Wakulima wengi wa Zanzibar hasa wale wa kilimo cha mboga, wameanza kuona ishara ya kupata utajiri kutokana na mapato makubwa wanayoyapata kupitia kilimo hicho kinachoendeshwa kwa kufuata ushauri wa kitaalamu. Ushahidi kutoka kwa wakulima mbali mbali wa kilimo hicho umeonesha kuwa wakulima wanao uwezo wa kukusanya hadi shilingi 20,000 kwa kila mche mmoja wa tungule ambao kuoteshwa kwake hadi kuvunwa kutafanywa kwa kufuata ushauri wa kitaalamu.

Kwa hesabu hiyo mkulima anao uwezo kuzalisha kwa uchache hadi Tsh. Milioni ishirini (20,000,000/=) kwa kulima tungule kwenye shamba lenye ukubwa wa nusu heka iwapo atapata mbegu bora, mbolea, maji ya kumwagilia na bila ya shaka usimamizi mzuri utakaomuwezesha kubaini maradhi ya mimea katika hatua za awali na kuyatibu.

Licha ya sehemu ya bidhaa za mboga kuendelea kuagizwa kutoka Tanzania Bara, wakulima wa Zanzibar wameonekana kufaidika zaidi na soko la Zanzibar kutokana na kuepukana na gharama za usafiri ikilinganishwa na wakulima wenzao kutoka Tanzania Bara hasa wale walioko nje ya Dar es Salaam.

Kwa upande wa uvuvi, imekuwa jambo la kawaidi hivi sasa kuzungumzia suala la ufugaji wa samaki Zanzibar, lugha ambayo katika miaka iliyopita ilikuwa haifahamiki miongoni mwa wananchi wa Zanzibar. Kazi za ufugaji wa samaki ambazo sasa ni maarufu katika visiwa vya Unguja na Pemba, imethibitika kuwa inaweza kuleta tija na kutoa ajira kubwa kwa wananchi, iwapo tatizo la upatikanaji wa vifaranga litapatiwa ufumbuzi.

Juhudi za Serikali katika kuleta mapinduzi ya kilimo na uvuvi zilianza kuonekana zamani kwa kuwekwa kwenye mipango mikuu ya kitaifa ikiwemo MKUZA I, II na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ambacho kimekuwa kikitawala tokea kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini mwaka 1992.

Miongoni mwa mkakati ambao serikali imekuwa ikiutumia ni kuwashirikisha washirika wa maendeleo kutoka nchi mbali mbali. Serikali ya Jamhuri ya Korea ni moja kati ya washirika wa karibu wa maendeleo ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukabiliana na changamoto ya umasikini na hasa katika kuimarisha kilimo ambacho ndio uti wa mgongo wa taifa.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein hivi karibuni alikutana na Balozi wa Jamhuri ya Korea Mhe. Song Geum-Young na kuzungumzia masuala mbalimbali ya uhusiano na ushirikiano ikiwemo masuala ya kilimo akiutaja msaada mkubwa wa serikali ya Jamhuri ya Korea katika kilimo cha umwagiliaji.

Katika mazungumzo hayo Dk. Shein na balozi Young walisifu jitihada za serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea za kuimarisha uhusiano uliopo tangu nchi mbili hizo zilipoanzisha uhusiano wa kidiplomasia kwenye miaka ya tisini.

"Tumefanya jitihada kubwa za kuimarisha uhusiano wetu na matokeo yake sasa nchi zetu zinashirikiana kwa karibu katika mambo mbalimbali katika nyanja za kidiplomasia, uchumi na maendeleo" Dk. Shein alimueleza Balozi huyo.

Alifafanua kuwa ushirikiano katika biashara na uwekezaji, elimu, afya na kilimo ambayo ni kati ya maeneo yaliyowekewa mkazo katika ushirikiano ni maeneo muhimu kwa kuwa yanasaidia jitihada za kupunguza kiwango cha umasikini hivyo kujenga ustawi wa wananchi.

Dk. Shein alibainisha kuwa chini ya uhusiano huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwemo Zanzibar imekuwa ikifaidika na misaada mbalimbali ambayo imekuwa chachu katika kuongeza kasi ya jitihada za wananchi wa Tanzania kujiletea maendeleo.

Katika mazungumzo hayo Dk. Shein aliishukuru Serikali na wananchi wa Jamhuri ya Korea kwa misaada yake kwa Serikali na watu wa Zanzibar na kuutaja mradi mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji kuwa moja ya matokeo makubwa ya ushirikiamo kati ya nchi hiyo na Zanzibar.

"Kupitia mradi huu wa umwagiliaji, tunatarajia kutimiza lengo letu la muda mrefu la kujitegemea kwa chakula hivyo ni habari njema kwetu kuwa taratibu za kuanza utekelezaji wa mradi huu zitakamilika hivi karibuni" Dk. Shein alieleza.

Pamoja na mradi wa kilimo cha umwagiliaji, Jamhuri ya Korea kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa (KOICA) inaisaidia pia Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Ulimwenguni (FAO) mradi wa ufugaji wa samaki wenye thamani ya zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 3.4.

Dk. Shein alitambua mchango wa shirika la kazi za kijamii la Korea la SAEMAUL ambalo alisema limekuwa likifanya kazi nzuri za kusaidia maendeleo ya jamii katika maeneo ya vijijini hapa Zanzibar.

Kwa upande wake Balozi wa Jamhuri ya Korea alimueleza Dk. Shein kuwa nchi yake inaupa kipaumbele uhusiano wake na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ingependa kuona unaimarika siku hadi siku.

Alifafanua kuwa ujumbe maalum wa nchi hiyo utakuja tena nchini kwa mazungumzo zaidi ya ushirikiano baada ya mkutano kama huo wa ushirikiano uliofanyika mwezi Aprili mwaka huu.

Balozi Young alieleza kufurahishwa kwake kuona zaidi ya vijana 80 wa kujitolea wa Kikorea wanashiriki hutoa huduma za kijamii katika sehemu mbalimbali za Tanzania ikiwemo Zanzibar. Alieleza kitendo hicho kuwa ni kilelezo kingine cha kuonesha na kuimarisha urafiki mzuri uliopo kati ya nchi yake na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika mkutano huo Balozi Young alimhakikishia Dk. Shein kuwa nchi yake itaendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutekeleza miradi yake ya maendeleo.

